epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Agosti 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581763
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 21
CHELSEA BADO YAMKOMALIA OSIMHEN



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiangalia bidhaa mbalimbali za kilimo zilizotokana na bustani wakati wa kilele cha maonesho ya wakulima Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma jana. Kulia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega. **Picha zaidi Uk. 8. PICHA: IKULU**

# Samia atoa sababu serikali kununua magari ya kifahari

• **Waliovamia** maeneo ya TARI 'kitanzini'... *Endelea ukurasa 2*



**Hadhari kwa watanzania wanaoishi Uingereza**
UKURASA 19

UKURASA WA 3
**WHO** yatoa hadhari kasi kuenea kwa UVIKO-19

UKURASA WA 4
**Baba** anavyosotea bima ya mwanawe aliyepata ulemavu wa kudumu



UKURASA WA 5
RIPOTI MAALUM - 2
**Uzoaji** taka ulivyogeuka kitendawili, tishio kiafya



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Mahitaji Maalum, Dk. Dorothy Gwajima

## Waziri ang'aka video 'hausigeli' kulisha wanafamilia haja kubwa

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAENDELEA KUINYANYASA SIMBA UK.24 **KATUNI** UK.6



Mfanyabiashara mdogo maarufu 'Machinga' akiwa amefunga banda lake kwenye vyuma vya kingo za daraja la magari akiendelea na shughuli zake, eneo la Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. Pamoja na kuwapo kwa soko la wafanyabiashara wadogo lililojengwa na Manispaa ya Ubungo karibu na kituo kikuu cha Mabasi cha Magufuli, bado baadhi yao wameendelea kufanya shughuli zao katika maeneo yasiyo rasmi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais Samia ataja sababu serikali kununua magari ya kifahari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza sababu ya serikali kununua magari ya kifahari na kwamba inafanya mambo yake kwa mujibu wa mipango.

Amesema kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiikosoa serikali kwa madai kuwa inanunua magari ya kifahari kwa ajili ya watendaji wake badala ya kununua matrekta.

Rais Samia alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima kitaifa Nanenane iliyofanyika katika Viwanja vya Nzuguni, mkoani Dodoma.

Aliwapongeza wakulima, wafugaji na wavuvi kwa mchango mkubwa ya kulilisha taifa, utoshelezi wa chakula na kwamba jasho na nguvu zao zina thamani kwa kuifikisha Tanzania kiwango cha kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 128.

"Nimekuwa nikisikia watu wanasema serikali inafuja fedha kwa kununua magari kwa ajili ya watendaji wake badala ya kununua matrekta kwa ajili ya wakulima, ndugu zangu serikali inafanya mambo yake kwa kuzingatia mipango yake haizuki tu, bila kununua magari ya watendaji tunayofanya yote ni bure nani atakwenda kusimamia," alisema Rais Samia.

Alisema, lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 serikali inapeleka matrekta 10,000 pamoja na power tiller 10,000 kwa wakulima.

"Vile vile serikali imeimarisha hivi sasa huduma za ugani pamoja na vitendea kazi na sisi serikali tumejenga maabara bora ya kilimo ambayo sampuli zote zitakuwa zinapita pale ifikapo mwaka 2026," alisema.

"Serikali imejipanga kujenga uchumi jumuishi unaowezesha kuwainua wananchi wote na unaowezesha kunufaika ipasavyo na jasho lao, ukweli ni kwamba wananchi wengi wapo kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvu ndio maana tuliongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 294 mwaka 2022/23 hadi Sh. trilioni 1.2 ikiwa ni ongezeko la mara nne na Shilingi trilioni moja ya nyongeza kwa ajili ya kuendeleza wakulima," alisema.

Alisema serikali ilitoa ahadi na imeonyesha nia kwa vitendo kwamba wakulima na wafugaji ni kipaumbele na kwamba uwekezaji umeleta mageuzi kuongeza matumizi ya mbolea, maeneo ya umwagiliaji maji, usambazaji mbegu bora na kuanzisha vituo jumuishi vya zana za kilimo.

Pia, alisema serikali imeendelea na jitihada za kuboresha sekta ya kilimo kwa kujenga majosho pamoja na kutafuta masoko ya bidhaa na kujenga viwanda vya uchakataji nyama kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

"Lakini pia kwa kushirikiana na taasisi za kifedha tunaendelea kuongeza utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu na naomba taasisi za fedha zote kuendelea na utaratibu huo," alisema.

Kuhusu jitihada zinazofanywa na serikali, alisema ni kujenga uchumi jumuishi na kuongeza tija katika mazao mbalimbali ikiwamo mpunga na mahindi.

Kadhalika, serikali imetafuta masoko yenye bei nzuri kwa mazao ya wakulima na kwamba zao la mbaazi halikuwa na thamani miaka mitatu minne iliyopita liliuzwa kilo Sh. 200 na sasa ni Sh. 4,000 huku kokoa ilikuwa ikiuzwa Sh. 700 hadi 900 na sasa ni Sh. 30,000, ikiwa ni kutokana na mbinu zilizofanywa ili kuwawezesha wajitegemee.

"Tunafanya yote haya kwa kudhihirisha kwamba serikali imedhamiria kujenga uchumi jumuishi kwa kuwezesha wakulima, wafugaji na wavuvi. Si kwamba tumemaliza matatizo yote, lakini tumepiga hatua kubwa mfano tija ya mchele imeongezeka tani 1.25 hadi tani nne kwa hekta na mahindi ilikuwa tani mbili na sasa ni 4.5. Lengo ni kufika tani saba kwa mpunga na mahindi tani tano," alisema.

"Hayo yamechangia kutuwezesha kiwango cha uzalishaji wa mazao ya chakula 17.1 msimu wa 2021/22 hadi tani milioni 20.4 mwaka 2023/24 ni ongezeko la asilimia 19, haya ni maendeleo makubwa kwa uchumi wetu.

"Mifugo uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho kwenye mashamba ya serikali umeongezeka kutoka tani 22.7 mwaka 2022/23 tani 127.7 mwaka 2023/24 huku vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kutoka tani 1.6 mwaka 2022/23 tani 1.9 mwaka 2023/24, uzalishaji wa mbegu za samaki umeongezeka kutoka tani 506,000 hadi 517,896 zenye thamani trilioni 3.34," alisema.

Rais Samia alisema serikali imeanzisha programu ya BBT kwenye uvuvi na wametoa mkopo kwa wa Sh. bilioni 1.1 kwa vikundi 25 kwenye sekta hiyo, lengo ni kupata chakula na kitoweo na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa, kutoa ajira na kupatikana malighafi za viwandani.

"Tukaoelekea mbele lengo la kujenga uchumi jumuishi ni kuongeza tija katika sekta za uzalishaji kwa kuongeza kipato kwa wananchi, tutaendelea kutengeneza ajira kwa vijana kujiajiri au kuajiriwa," alisema Rais Samia.

Awali, Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, alisema Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), inaitaka wizara hiyo ifikapo 2025/26, sekta hiyo iwe imefikia asilimia 130.

Alisema katika mauzo yatokanayo na mazao ya kilimo wamepanga kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka huu kutoka mauzo ya Dola za Kimarekani bilioni 2.3 za mwaka jana.

Utaratibu wa serikali kutoa ruzuku ya mbolea umesaidia kuongeza matumizi kutoka tani 360,000 hadi 900,000.

Kadhalika, alisema wizara yake inakwenda kuwatoa watu wote waliovamia maeneo ya serikali hususani ya kilimo.

"Mheshimiwa Rais tunakwenda kuwatoa wote waliovamia maeneo ya serikali hususani yale ya kilimo ya Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI) na Nanenane kwani uvamizi wa maeneo ya serikali umefika mwisho," alisema.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema kutokana na changamoto ya ugonjwa wa kideri ambayo imekua ikiwakabili wafugaji wa kuku, na kwamba katika kukabili jambo hilo mwaka huu wamepanga kutoa chanjo bure.

Alisema pia wizara hiyo mwaka huu imepanga kuendelea kukopesha wavuvi boti 450 pamoja na vizimba vya ufugaji samaki 900.

## Ma-RC, ma- DC wapewa maagizo mazito

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKUU wa mikoa na wilaya nchini, wametakiwa kusimamia matumizi ya vifaa vya kilimo vinavyonunuliwa na serikali ili vitumike kwa ajili ya shughuli zinazolengwa na kusaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema hayo jana alipokuwa anafunga Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye ulemavu, Ridhiwan Kikwete

Majaliwa aliwataka viongozi hao kuwasimamia maofisa ugani na maofisa kilimo wa maeneo yao ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ya kutoa elimu ya kilimo bora kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji.

Pia aliwataka viongozi hao kusimamia maeneo yote yenye miundombinu ya umwagiliaji ili yatumike vizuri kati ya wakulima na wafugaji bila kuibua migogoro.

Waziri Mkuu aliitaka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inapoandaa maandiko ya skimu za umwagiliaji kwenye maeneo ambayo kuna wafugaji, ihakikishe zinawanufaisha pia wafugaji kwa kuwaandalia maeneo ya kunyweshea mifugo. "Lakini pia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwawezeshe wafugaji kupata chakula bora cha mifugo hasa samaki ili kuongeza tija kwenye uzalishaji na msaidiane kudhibiti migogoro kati ya wakulima na wafugaji," alisema Majaliwa.

Aidha, aliagiza shule zenye maeneo makubwa zipande mazao kama maharage lishe na matunda mbalimbali ili kuimarisha lishe kwa wanafunzi huku akisema mikoa yenye uzalishaji mkubwa wa chakula ndiyo yenye viashiria vingi vya udumavu wa watoto.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, aliwataka wafugaji wote nchini kuzingatia sheria katika maeneo yote ambayo wanaishi ikiwamo kuepuka kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima, hali ambayo husababisha migogoro na wakulima.

Pia aliwataka wafugaji kufuga mifugo yao kisasa ili kuongeza tija ya mifugo hiyo ikiwamo kuboresha bei ya mifugo na mazao yake ili sekta hiyo iwe moja ya sekta zinazoongoza kwa kuliingizia taifa mapatao. Alisema mfugaji yeyote kama anataka kufuga ni lazima awafuate viongozi wa serikali za vijiji na mitaa ili wampatie eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo kwa maelezo kuwa kwa sasa asilimia kubwa ya vijiji nchini vimewekewa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Alisema utaratibu wa wafugaji kuhamahama na makudi ya mifugo hautakiwi badala yake wafugaji wanatakiwa kuchangia kwenye maeneo yeliyotengwa. "Sisi wizara tunaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji wa malisho, kugawa mbegu za malisho bora kwahiyo sisi kama Wizara hatutakuwa sehemu ya kuwatetea wafugaji wasiofuata sheria," alisema Mnyeti.

Alisema takwimu za mifugo zinaonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la mifugo nchini akidai kuwa mpaka kufikia mwaka wa Fedha 2023/2024 Tanzania kuna ngombe milioni 37.9, mbuzi milioni 27.6, kondoo milioni 9.4, nguruwe milioni 3.9 na kuku milioni 100.3.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mikoa hiyo imekuwa ikiongoza kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali hasa ya chakula, hivyo kuwa sehemu ya mikoa inayolisha taifa.

Alisema uzalishaji umekuwa ukiongezeka kutokana na serikali kuweka ruzuku kwenye mbolea na elimu ya kilimo bora ambayo wakulima wamekuwa wakiipata mara kwa mara.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Daniel Sillo akiwahutubia wakimbizi kutoka nchini Burundi, waliopo katika kambi ya Nduta, wilayani Kibondo, mkoani Kigoma juzi, kuhusu umuhimu wa urejeaji wa hiari nchini mwao, wakati wa kampeni ya "njoo utuambie" yenye lengo la kuhamasisha wakimbizi warudi nchini kwao, iliyoishirikisha Serikali ya nchi hiyo na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR). **PICHA: ADELA MADYANE**

# Waziri ang'aka video 'hausigeli' kulisha wanafamilia haja kubwa

**Na Romana Mallya**

VIDEO inayomwonesha msichana akidai kulisha wanafamilia chakula kilichochanganywa na haja kubwa na ndogo, imemwibua Waziri Dorothy Gwajima, akiagiza kuchukuliwa hatua dhidi ya waliomwajiri mtoto huyo kufanya kazi za ndani.

Waziri huyo wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum amesema ajira kwa mtoto huyo, pia kupigwa picha mjongeo na kusambazwa mitandaoni, ni unyanyasaji, hivyo waajiri wake wasakwe ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Juzi kulisambazwa kipande cha video katika mitandao ya kijamii, kikimwonesha msichana huyo ambaye hajavuka umri wa utoto, akihojiwa na waajiri wake - mwanamume na mwanamke, wakimtuhumu kufanya "vitendo vichafu" ndani ya nyumba yao.

Wakati wa mahojiano hayo ambayo zaidi yalifanywa na mwanamume, wanamwuliza maswali kadhaa kuhusu vitendo anavyofanya katika nyumba yao hiyo; naye anajieleza kuwa amekuwa akiweka haja kubwa katika chakula.

Vilevile, mtoto huyo anadai amekuwa anaweka haja ndogo katika chai, kutemea mate maji ya kunywa anapoagizwa kuwapatia wanafamilia na amekuwa akitoka nyumbani kwenda kuingiliwa kinyume cha maumbile na madereva wa pikipiki za kubeba abiria, maarufu bodaboda.

Muda mfupi baada ya kusambazwa kipande hicho cha video, Waziri Dorothy alikemea na kulaani kitendo cha waajiri hao kumrekodi binti huyo na kusambaza video mitandaoni.

Dk. Dorothy pia alisema kitendo cha kumwajiri mtoto huyo kinakiuka sheria. Ni utumikiswaji watoto unaokatazwa kisheria - Sheria ya Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2009 na mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeridhia kulinda haki za watoto.

Katika taarifa yake jana, Dk. Dorothy alisema: "Hivi karibuni, kuna video imesambaa katika mitandao ya kijamii ikimwonesha binti ambaye ni msaidizi wa kazi za ndani akihojiwa na waajiri wake kuhusu tuhuma za kuwalisha chakula kichafu na kuchafua nguo za watoto anaowalea katika familia hiyo. "Wizara inakemea na kulaani kitendo cha kumhoji, kupiga picha na kusambaza katika mitandao ya kijamii, kwani ni kinyume cha Sheria ya Mtoto Sura ya 13 Sehemu ya 33(1),:

Waziri Dorothy alisema kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha sheria hiyo ya mtoto, ni kosa la jinai kumwajiri mtoto kwa shughuli yoyote inayoweza kuwa na madhara kwa afya yake, elimu yake na afya yake ya akili au makuzi yake kimaadili.

Alisema adhabu ya kosa hilo chini ya kifungu cha 14 cha sheria hiyo ni kifungo cha hadi miezi sita gerezani na faini ya hadi Sh. milioni tano au kifungo na faini kwa pamoja.

"Nitumie fursa hii kuwaasa wananchi wote kutofumbia macho vitendo hivi na kutoa taarifa ya matukio kama haya katika Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zilizoko katika kila mtaa, kijiji, kata na ofisi za ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo vya Jeshi la Polisi," Dk. Dorothy alisema.

Waziri huyo alisema taarifa kuhusu tukio hilo zitawezesha hatua za kisheria kuchukuliwa haraka, akiomba wananchi wenye taarifa sahihi za mkoa, wilaya, mtaa na makazi ambako tukio hilo limetokea watoe taarifa kwa utaratibu alioeleza awali.

Dk. Dorothy pia alitaka jamii kuzingatia sheria na maadili katika kushughulikia suala lolote linalohusu mtoto.

# WHO yahadharisha kasi kuenea UVIKO-19

**Na Moshi Lusonzo**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limehadharisha kuhusu maambukizi ya virusi vipya vya Uviko-19 huku likisema ni hatari na vinasambaa kwa kasi.

Akizungumza na vyombo vya habari nchini Uswis juzi,

Mkurugenzi wa WHO wa Maandalizi ya Kinga na Magonjwa ya Mlipuko na Majanga, Dk. Maria Van Kerkhove, alisema juzi Geneva, Uswisi kwamba maambukizi hayo mapya yameripotiwa katika nchi mbalimbali duniani.

Alisema uchunguzi uliofanyika katika nchi 84, imegundulika katika sampuli za vipimo vilivyochukuliwa, asilimia 10 zina virusi hivyo, huku nchi za Ulaya zikiongoza kwa asilimia 20.

Dk. Van Kerkhove alisema viwango hivyo vya kusambaa kwa virusi vya UVIKO-19, vinabadilika kwa viwango kwa kila nchi jambo ambalo ni hatari.

Alisema virusi vya UVIKO-19 vinabadilika na kuwa vikali zaidi, hivyo kusababisha idadi ya watu wanaolazwa hospitalini kuongezeka katika nchi nyingi.

Kutokana na kasi hiyo, alisema WHO imetoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukua ambayo nchi zote duniani zimetakiwa kutekeleza ili kuepuka maambukizi mapya ya ugonjwa huo.

Shirika hilo limezitaka serikali na watu binafsi kuchukua hatua kupunguza athari kwa kuweka misingi bora ya kupambana na ugonjwa huo. Pia limezishauri serikali kuwapa wananchi zana za kujilinda na kuwatunza watu walioathirika.

Pendekezo lingine, nchi zote zitumie mbinu mbalimbali kuwagundua na kuripoti wagonjwa wanaofikishwa hospitalini na kutathmini hatari na ukubwa wa tatizo.

Aidha, nchi zimetakiwa kutathmini utayari wa mifumo ya kukabiliana na maambukizi ya virusi hivyo na kwamba watu wasikae wakijua ugonjwa umekwisha bali waendelee kupata chanjo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Jerry Khanga, alisema katika miaka miwili, utoaji wa chanjo umepungua, hivyo kutokana na ripoti hiyo, kuna umuhimu watu kuendelea kuchanja na wale waliopata wapewe ya chanjo ya pili.

# 49 watiwa mbaroni madai ya uhalifu wa nyumbani, ujangili

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa limewakamata watuhumiwa 49 wa makosa mbalimbali ya kihalifu, ukiwamo uvunjaji, uwindaji haramu, utapeli na matumizi ya dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Allan Bukumbi, watuhumiwa hao walikamatwa wakati wa operesheni na msako wa wahalifu.

Alisema mbali na watuhumiwa hao, kuna kesi ambazo Jeshi la Polisi limepata mafanikio kwa washtakiwa kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo na wengine kulipa fidia.

"Jeshi la Polisi limemkamata Faustine Salesi (45), mkulima na mkazi wa Pawaga, akiwa na wenzake wanne wakiwa na bunduki mbili aina ya gobore, silaha nyingine za kienyeji ambazo ni visu, panga na shoka pamoja na nyara za serikali ambazo ni nyama ya swala, digidigi na ngiri.

"Silaha hizo wamekuwa wakizitumia katika matukio mbalimbali ya ujangili katika Hifadhi ya Taifa Ruaha," alisema Kamanda Bukumbi.

Alisema jeshi hilo limekamata mtuhumiwa aitwaye Ujuzi Msangailwa (22), mkulima na mkazi wa Nyakavangala akiwa na mawe matatu ya madini ya dhahabu bandia, eneo la Kituo Kikuu cha Daladala Kata ya Makorongoni, Manispaa na Mkoa wa Iringa ambayo alikuwa akiyatumia kutapeli watu katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Iringa, akiwarubuni kuwa ni madini. Inadaiwa ametoka nayo Nyakavangala.

Kamanda Bukumbi alisema wamemkamata Bashir Lupondo (18), dereva bajaji na mkazi wa Makorongoni na wenzake kumi (10), wakiwa na misokoto 257 ya bangi katika debe.

"Moja ya mafanikio tuliyopata kwenye kesi ambazo zilifikishwa mahakamani ni kwa watuhumiwa saba kutiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu mbalimbali vikiwamo vifungo na wengine kulipa fidia," alisema Bukumbi.

Alitaja watu hao kuwa ni Mwasema Rashid (37), fundi bomba, mkazi wa Dar es Salaam, aliyehukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kwa kumeza kete 58 akitokea Zambia kuelekea Dar es Salaam.

Wamo pia Moses Kidago, mkulima na mkazi wa Idodi, aliyehukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani kwa kosa la kupatikana na nyara za serikali katika Hifadhi ya Taifa Ruaha; Bariki Likolongo (58) mfugaji na mkazi wa Idodi ayehukumiwa kifungo cha miezi minne au kulipa fidia Sh. 500,000; na Laiton Yeganise (30) mkulima na mkazi wa Kihesa aliyehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja gerezani, wote wawili kwa kosa la wizi wa mabomba ya madaraja eneo la Wenda katika mradi wa barabara ya Ihemi-Mgama.

Wengine ni Thomas Nyato (21), mkulima wa Mgololo, aliyehukumiwa kifungo cha miaka mitano jela, Mussa Nziku (28), mkulima wa Kinyanambo, aliyefungwa miaka mitatu na Chaguzi Magoda (47), mkulima wa Luganga, aliyehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja, wote kwa kosa la kuua bila kukusudia.

"Kwa upande wa doria na misako inayoendelea kufanyika, tumemkamata mtuhumiwa wa matukio ya uvunjaji, Raymond Kalolo (27), mkulima na mkazi Frelimo Manispaa ya Iringa na watuhumiwa wengine (31) wakiwa na mali mbalimbali za wizi ambazo ni pikipiki sita, godoro chakavu, mafuta lita 60 yanayotumika katika minara ya simu, presure cooker mbili, spika kubwa moja, baiskeli ndogo nne, vitasa vya madirisha ya vioo 78, runinga tatu za inchi32, aina ya hometech na aborder, microwave mbili na sabufa aina ya sea piano nne," alisema.

# Baba asotea bima ya mwanawe aliyepata ulemavu wa kudumu

**Na Benny Kingson,** TABORA

BABA wa mtoto Raphael Mdaki (6), Mrisho Mdaki, mkazi wa kijiji cha Isikizya, Uyui, mkoani Tabora, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati suala la kulipwa fidia ya bima kutokana na kuzungushwa kwa muda mrefu baada ya ajali ya gari kumsababishia ulemavu wa kudumu mwanawe.

Inadaiwa kuwa mtoto Raphael aligongwa miguu na gari aina ya Scania lenye namba za usajili T396 ADB, la Kampuni ya ATTT lililokuwa limebeba kokoto na kusababisha miguu yote kukatwa lakini mpaka sasa, hajalipwa fidia licha ya kudai kutumia fedha nyingi kwenye matibabu ya mtoto huyo.

> **"Tulifuatilia madai ya fidia kwa mwajiri wa dereva kwa kutumia wakili ambaye aliandika madai ya Sh. milioni 50 ambako mmiliki huyo wa gari alitekeleza kwenda......**

Akizungumza mwandishi wa habari hii, Mdaki alisema tukio hilo lilitokea Februari 10, 2023 katika barabara kuu itokayo wilayani Nzega wakati gari hilo likienda Tabora mjini.

Alisema gari hilo lililokuwa likiendeshwa na Juma Kasenye (29) lilimgonga mtoto wake majira ya saa 8:50 mchana.

"Gari hilo lilitanguliwa na magari mengine matatu ambayo yote yalimpita mtoto wangu akiwa pembeni mwa barabara lakini lori hilo lilipomfikia lilimburuza na matairi ya nyuma yakamkanyaga miguu yote miwili na kusababisha kukatwa na sasa ana ulemavu," alisema.

Mdaki alisema walifungua shauri lenye namba 4/2023 la Makosa ya Usalama Barabarani katika Mahakama ya Wilaya ya Uyui Februari 21, 2023 na dereva huyo Kasenye alikutwa na hatia, hivyo kutozwa faini ya Sh.30,000 na kulipa kisha kuachiwa.

Alisema familia iliendelea kumtibu mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora, Kitete kwa gharama zao.

"Tulifuatilia madai ya fidia kwa mwajiri wa dereva kwa kutumia wakili ambaye aliandika madai ya Sh. milioni 50 ambako mmiliki huyo wa gari alitekeleza kwenda jijini Mwanza ambako kuna ofisi za bima yake kubwa,' alisema.

Alisema Septemba, 2023 walikwenda jijini Mwanza katika ofisi za bima na kutakiwa kurejea nyumbani Tabora hadi watakapopata taarifa na baada ya muda walipigiwa simu wakitakiwa kupeleka nyaraka zinazoonyesha mtoto ameumia kwa kiwango gani.

"Tuliwapelekea nyaraka ikionesha mtoto ameumia kwa asilimia 100 na walituambia watawasiliana na ofisi yao makao makuu Dar es Salaam na baada ya muda, nikapigiwa simu wakaniuliza wanitumie Sh. milioni tano za fidia, niliwakatalia na nikawaambia pesa hiyo haitoshi kwa kuwa mtoto wangu wamemsababishia ulemavu wa kudumu," alisema.

Mdaki alisema baada ya kuona mambo yanakuwa magumu, walirudi kwa mmiliki wa kampuni hiyo kutaka kujua hatima yao na kubainisha kuwa wamekuwa wakizungushwa na kuambiwa walikwishapelekwa katika ofisi za bima ili walipwe, hivyo hawako tayari kuzungumza nao.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali na wadau wengine wenye mapenzi mema watakaoguswa na suala hilo, kumsaidia kupata haki zao kwa kuzingatia mtoto huyo kwa sasa anaishi katika mazingira magumu kutokana na ulemavu aliopata.

Pia alimwomba Rais Samia kuingilia kati sakata hilo ili mtoto wake aweze kupata malipo yake yote pia aweze kupata elimu na fedha za kumsaidia katika maisha yake.

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Kanda ya Ziwa, Richard Cheumbe, alipoulizwa kuhusu ucheleweshwaji wa malipo ya fidia kwa waathirika wa ajali za barabarani na viwango vya fidia, alisema hutofautiana kulingana na tukio husika.

Alisema ikitokea kuna kuchelewa inaweza kutokana na taratibu za ufuatiliaji ili kuhakikisha hatua zote za kisheria zinafuatwa.

Kuhusu viwango vya fidia, alisema inategemeana na tathimini na kuwa mara nyingi waathirika wa ajali huwa na mategemeo ya kupata fedha nyingi, hivyo kupokea fidia tofauti na uhalisia.

# Wakulima wakopeshwa trilioni 1.8/

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya CRDB imesema katika msimu huu wa kilimo imeshakopesha zaidi ya Sh. trilioni 1.81 ambazo ni sawa na asilimia 43 ya mikopo yote ya kilimo iliyotolewa na taasisi za fedha kwenye sekta ya kilimo nchini.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela wakati mgeni rasmi wa kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima, Nanenane Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea banda la benki hiyo jijini Dodoma jana.

Nsekela alisema kwa miaka mitatu iliyopita, hadi Julai 2024, Benki ya CRDB imekopesha jumla ya Sh. trilioni 4.06 kwenye sekta ya kilimo na Sh. bilioni 944.6 kati ya kiasi hicho, zimeelekezwa kwenye vyama 541 vya ushirika (AMCOS) kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo, ujenzi wa maghala na viwanda vya kuchakata mazao, ufugaji, uwekezaji kwenye misitu na uvuvi.

"Kwenye sekta ya mifugo na uvuvi, mpaka Julai 2024, Benki ya CRDB imekopesha Sh. bilioni 70 na tumeingia makubaliano na Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kutoa mikopo kwa wanachama wake ili wafuge kwa tija kwa kuweka miundombinu ya kunyweshea na kulima chakula cha mifugo.

"Kule Zanzibar, Benki ya CRDB inatekeleza mpango maalum wa 'Inuka na Uchumi wa Buluu', ambao hadi Julai 2024, imeshakopesha zaidi ya Sh. bilioni 29 kwenye Programu ya Inuka kwa wajasiriamali na Sh. bilioni 28 kwenye uchumi wa buluu," alisema Nsekela.

Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Nsekela alisema Benki ya CRDB imeshiriki kujenga mfumo wa kidigiti wa usajili wa wakulima na usambazaji mbolea ya ruzuku.

Mfumo huo, Nsekela alisema unatumika kusajili wakulima, waagizaji, wazalishaji wa mbolea na mawakala.

"Mfumo huu wa usajili wa wakulima unahusiha upatikanaji kadi janja yenye kuwawezesha wakulima kufanya miamala ya kibenki (financial services) na huduma mbalimbali za kidigiti, ukiwamo utambuzi wa mkulima wakati wa uchukuaji ruzuku siku za usoni," alisema Nsekela.

Ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa, mkurugenzi huyo alisema kampuni tanzu yake ya bima ya CRDB Insurance Company (CIC) inatoa bima ya mifugo inayotumia teknolojia ya kisasa ya kutambua pua ya mfugo kama ilivyo kwa alama za vidole kwa binadamu.

"Hii inatuwezesha kuwakopesha wafugaji kwa kutumia dhamana ya mifugo yao," alisema Nsekela.

Nsekela pia alitumia nafasi hiyo kuelezea Programu ya Imbeju inayotekelezwa na taasisi yake ya CRDB Bank Foundation ikijikita kuwezesha vijana, wanawake na makundi maalumu, wakiwamo wakulima na wafugaji kwa kuwapa elimu ya fedha na mafunzo ya ujasiriamali.

Programu hiyo ambayo hutoa fursa ya kuwafungulia akaunti washiriki wa mafunzo, tayari imenufaisha zaidi ya watu 500,000 kwa mtaji wezeshi iliyoitoa mpaka sasa ambayo ni Sh. bilioni 10.

Taasisi ya CRDB Bank Foundation pia inashirikiana na taasisi ya Sokoine University Graduate Entrepreneurship Cooperative (SUGECO) kuwezesha wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo nje ya nchi.

Katika utaratibu huu, kila mnufaika anapata mtaji wezeshi wa kati ya dola 3,500 za Marekani (Sh. milioni 8.7) mpaka dola 4,500 (Sh. milioni 11.29).

Zaidi ya wahitimu 2,500 wanatarajiwa kunufaika na ushirikiano huu na wakirejea nchini upo utaratibu wa kuwawezesha kuwekeza katika kilimo cha kisasa na kuuza mazao yao ughaibuni.

Vilevile, CRDB Bank Foundation ina makubaliano na kampuni ya Tanzania Breweries Limited (TBL) kutoa elimu ya fedha na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa wakulima wadogo wa shayiri na kuwajumuisha rasmi katika mfumo wa benki.

"Tayari wakulima 64 wamenufaika na zaidi ya shilingi milioni 325 zimetolewa kama mtaji wezeshi na kupatiwa bima ya mazao. "Vilevile, tumeingia makubaliano na kampuni ya Kagera Sugar na Kilombero Sugar zinazoturuhusu kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo wa miwa (outgrowers), kuwapa mitaji wezeshi ya kununua mbegu, viwatilifu na kukidhi mahitaji mengine muhimu. Na tunawapa bima ya mazao pia," alisema Nsekela.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA GEITA NA KAGERA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza mzunguko wa pili ulianza kufanyika tarehe 5 katika Mikoa ya Geita na Kagera na utahitimishwa tarehe 11 Agosti, 2024 na kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Uboreshaji ulianza kufanyika siku ya Jumatatu tarehe 05 na utahitimishwa tarehe 11 Agosti, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuwani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa tarehe 07 Agosti, 2024 na:**

Christina Ballali
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI



hosplan

**Job Opportunity: Health Executive**

**Location:** Dar Es Salaam | Position: **Full-Time**
We are a leading global healthcare services company looking for a dynamic, energetic, and well-mannered Health Executive to engage with high-end clientele and guide them through accessing advanced medical treatments across the world.

**Key Qualifications:**
- Minimum graduation; healthcare background preferred.
- Good schooling and education background.
- Strong communication and interpersonal skills.
- Ability to engage with high-end society and provide personalized support.

**Benefits**:
- Competitive compensation.
- Opportunity to work with a prestigious clientele.
- Professional development and growth opportunities.

**How to Apply:**
Submit your resume to **amit@hosplan.com** / WhatsApp:- **+255748555889**
Application Deadline: **16th August 2024**

**www.hosplan.com**
***Treatment Traveller Tanzania Limited***

RIPOTI MAALUM -2

# Uzoaji taka ulivyogeuka kitendawili, tishio kwa afya

SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii, ilieleza uondoshaji taka katika mitaa ya Jiji la Mwanza ulivyo kitendawili kigumu kwa mamlaka hiyo. Pia wananchi walieleza madhila wanayopata kutokana na tatizo hilo, yakiwamo magonjwa ya mlipuko. Endelea...



Taka zikiwa zimezagaa katika moja ya mitaa ya Jiji la Mwanza. **PICHA: VITUS AUDAX**

---

KWA mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kifungu cha makosa yanayohusu Uchafuzi wa Mazingira Na. 187(1), mtu yeyote ambaye (a) atamwaga vitu vyovyote vya hatari, mafuta, michanganyiko ya mafuta kwenye ardhi, maji, hewa au mazingira oevu, ametenda kosa na adhabu yake ni kutozwa faini isiyopungua Sh. milioni tatu na isiyozidi Sh. milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka 12 gerezani au vyote viwili kwa pamoja.

Kifungu kidogo namba (2) kinaeleza kuwa pamoja na adhabu yoyote ambayo Mahakama inaweza kutoa kwa mtu aliyetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu cha (1), Mahakama inaweza kumwamuru mtu huyo (a) kulipa gharama zote za kusafisha mazingira yalivochafuliwa na kuondoa uchafu.

Swali la kujiuliza mamlaka za serikali za mitaa zinafanya hivyo? Je, wanatambua kuwapo sheria hiyo?

Kifungu cha 114(a) cha Usimamizi wa Taka Ngumu, kifungu kidogo namba (1) kinasema ili kuhakikisha taka ngumu zinapunguzwa kufikia kiwango cha chini katika maeneo yaliyo chini ya mamlaka yake, serikali za mitaa zinatakiwa kuagiza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na (a) kwa aina tofauti za taka, takataka, mabaki au uchafu, zichambuliwe na kutenganishwa kwenye chanzo chake; (b) kuweka viwango vya kuongoza aina, saizi, umbo, rangi na vipimo vingine kwa ajili ya taka zinavyotumika.

Vilevile (c) kuweka utaratibu kwa kushirikisha viwanda na sekta binafsi na asasi zisizo za kiserikali katika kupanga, kukuza weledi miongoni mwa wazalishaji, wachuuzi, wasafirishaji, watengenezaji viwandani na watu wengine kwa nia ya kupata jaa zinazofaa kwa taka na utenganishaji wa taka kwenye chanzo.

Kifungu kidogo namba (2) kinazitaka Mamlaka za serikali za mitaa kwenye maeneo yake kufanya mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na (a) kuhakikisha tathmini ya athari kwa mazingira inayofaa inafanyika kwa ajili ya shughuli zote kuu mpya zinazolenga kwenye usimamizi unaostahili wa taka ngumu;

(b) Zitasimamia taka ngumu zinazozalishwa kwa mujibu wa mipango endelevu iliyotolewa na serikali za mitaa husika; na (c) zitahakikisha uchambuzi wa taka unaostahili unafanyika pale kwenye chanzo na unazingatia viwango au vipimo vilivyoagizwa na serikali husika ya mitaa.

### SHERIA INAFUATWA?

Wadau mbalimbali wa mazingira wanasema kwa asilimia kubwa, jijini Mwanza hatua za muhimu kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira zimekuwa hazifuatwi hali inayosababisha ongezeko la takataka katika mitaa na makazi ya watu, hivyo kutishia afya za binadamu.

Katibu Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Synergistic Globe, Angelina Manyama, ambaye pia ni mkufunzi wa kozi ya uandishi wa habari za mazingira , Idara ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Mwanza, anasema kuna umuhimu wa serikali kuzibana idara zinazohusika ili kutekeleza matakwa ya sheria hiyo.

Anasema katika shughuli za utekelezaji wa afua za mazingira kumekuwa na milolongo mirefu inayosababisha baadhi ya wadau kuendelea na programu husika, ikiwa ni pamoja na ushirikiano mdogo wa wananchi kwa wadau husika.

"Tumekuwa tukijitahidi kutoa elimu kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira, tunaongea na viongozi mbalimbali kuhakikisha unawekwa utaratibu mzuri katika ukusanyaji taka lakini likija suala linalohusisha fedha inakuwepo mizunguko mingi hadi wadau wanasitisha utekelezaji wake kwa kukosa ushirikiano wa kutosha," anasema.

### OFISA MAZINGIRA JIJI

Akizungumza kwa njia ya simu kuhusu tatizo hilo, Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Fanuel Kasenene, licha ya kuthibitisha kuwapo kwa tatizo la utupaji taka ovyo, anasema ongezeko hilo husabibishwa na kukua kwa shughuli za kiuchumi sambamba na ongezeko la watu.

Anasema jiji hilo kushika nafasi ya mwisho katika matokeo ya Wizara ya Afya inatokana na wingi wa watu na si kwamba ni chafu kiasi hicho. Anasema sheria inamtaka mzalishaji wa kwanza wa taka kuwa na chombo maalum cha kuhifadhia taka na si kuzitupa.

"Mwanza Jiji na Ilemela pekee tuna zaidi ya watu milioni moja na wote hao wanazalisha taka na ukiona sehemu taka zinazalishwa kwa wingi jua kuna shughuli za kiuchumi zinaendelea. Ukisema tuishi bila kuzalisha taka inamaanisha hiyo jamii imekufa cha msingi ni kuwa tunawekaje mikakati ya kila mtu kushiriki kwenye nafasi yake kwa hilo suala siyo la serikali tu bali hata mzalishaji sheria inamtaka awajibike," anasema Kasenene.

Alisema kwa Jiji la Mwanza pekee zinazalisha takataka zaidi ya tani 357 kwa siku na kwa siku wanazoa tani 265 katika maeneo yote kupitia magari ya halmashauri aliyoyataja kuwa yanapita kwenye kata zote 18.

Kwa mujibu wa takwimu za ofisa huyo wa mazingira, zaidi ya tani 92 za taka zinazozalishwa kwa siku hazizolewi sawa na tani 2,576 kwa mwezi katika Halmashari ya Jiji la Mwanza pekee, hivyo kuwa sehemu ya taka zinazosumbua na kuhatarisha afya za wananchi.

Kuhusu maeneo ya kukusanyia taka yanayotakiwa kupangwa na serikali za mitaa, Kasenene alisema maeneo hayo yalikuwepo na kwa Jiji zima akitaja vituo kuwepo 22 na kuwa tatizo ni watu kulazimisha kutupa taka kwenye maeneo yasiyo ruhusiwa na wengine kutupa kwenye vyanzo vya maji.

"Sweya walikuwa na eneo karibu na SAUT. Eneo lingine liko ndani ya chuo na maeneo mengine kama Nyegezi kona na Luchelele lakini tatizo wazalishaji hawataki kufuata utaratibu.

Wakishazalisha wanatupa taka zao ovyo, wanapeleka kwenye saiti na kwenye sehemu za mito kwa sababu hawataki kufuata utaratibu," anasema Kasenene.

Kadhalika, Kasenene anathibitsiha kutokuwapo wazabuni maalum kwa ajili ya kuondosha taka hizo katika makazi ya watu na kuwa wako kwenye mchakato wa kutangaza zabuni ili kusaidia katika zoezi hilo.

### CHANZO MAWAKALA

Ofisa Mazingira, Kasenene anasema maeneo mengi jijini humo yamekuwa na mawakala wa kuzoa takataka kutoka kwenye makazi ya watu kupeleka katika vituo maalum, lakini tatizo kubwa limekuwa ni ushirikiano mdogo kutoka kwa wananchi wenyewe.

Anasema uendeshaji wa taka hizo ngumu una gharama hivyo wananchi hawataki kushiriki kulipia ushuru wa kuzoa taka kwa mujibu wa sheria

Katika kuzoa taka hizo, anasema kuna gharama zinazohitajika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mafuta kwa ajili ya magari, ukarabati wa magari, vifaa vya kusafisha, gharama za usafirishaji, kulipa wafanyakazi na vibarua wanaotoa huduma pamoja na mawakala wanaosimamia kazi hiyo hivyo wananchi kutakiwa kuchangia gharama hizo.

"Gharama wanazotakiwa kuchangia wananchi zinategemea na aina ya biashara wanazozifanya na kaya husika kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Mazingira kwa halmashauri ya Jiji ya 2017 kwa ya mjini katikati ni Sh.5,000 kwa kaya na maeneo ya pembezoni ni Sh.3,000 kwa mwezi.," anasema Kasenene.

Pia anasema baadhi ya masuala ya namna hiyo wananchi wanatakiwa kuwashirikisha viongozi wao wa mitaa na kata ili kupata njia sahihi za kukabiliana na kero hizo za taka.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maonesho Nanenane yamnufaishe mkulima

**WATANZANIA** jana wameadhimisha Sikukuu ya Nanenane ambayo kila mwaka hufanyika mwezi wa nane tarehe nane.

Maadhimisho haya hukutanisha wakulima wakubwa na wadogo kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania ambao hubadilishana uzoefu na kupata elimu ya kilimo bora.

Sherehe hizo hutoa fursa kwa wakulima wadogo kujifunza kutoka kwa wakubwa kwa lengo la kukifanya kilimo nchini kuwa na tija, na uzalishaji bora.

Hakika sherehe hizi hubadili mandhari ya maonesho na kufanya kuonekana kuwa kijani kutokana na mazao yanayostawishwa kwa kuzingatia njia bora za kilimo.

Kilimo cha kisasa na kile cha asili kinatofauti kubwa. Mathalani, cha asili kilikuwa kikizingatia mbegu za asili ambazo pamoja na mazao yake kuwa na ladha nzuri, lakini hayatoi mazao mengi.

Kwa kilimo cha kisasa ambacho kinatumia mbegu za kisasa zinazozalishwa kisasa, zinatoa mazao mengi na kinatoa mazao mengi katika sehemu ndogo ya ardhi na kwa muda mfupi.

Kumekuwapo na masomo ya mashamba ambayo huonesha jinsi kilimo cha kisasa kinavyosaidia kuzalisha mazao mengi na kwa muda mfupi hali inayosaidia kukabiliana na tatizo la njaa.

Sikukuu ya Nanenane huonesha pia ufugaji wa kisasa kuanzia wa kuku hadi wanyama na tofauti kubwa huonekana kati ya ule wa asili na wa sasa.

Kwa ujumla, maonesho ya Nanenane hutoa fursa kubwa ya wakulima kujifunza mpaka kwenye ufugaji wa samaki ambao kwa sasa umepamba moto na kutoa matokeo bora.

Wakulima hufundishwa jinsi ya kufuga kwa kutumia eneo dogo, ambalo hutoa mazao mengi na kuleta faida kubwa kwa mfugaji.

Kuna utaalamu wa kufuga samaki kwa kutumia matangi ya maji ambayo hukatwa katikati na kuokoa mtu kutumia eneo kubwa.

Ufugaji huu pia humsaidia mtu asiyekuwa na nafasi ya kutosha kwenye eneo lake kuendelea kufaidi matunda ya ufugaji na kupata kipato kinachomwezesha kumudu maisha ya kila siku.

Kwa wakulima na wafugaji, Siku ya Nanenane ni muhimu kwao kuendelea kupata ujuzi na kubadilishana uzoefu kwa wenzao waliopiga hatua na kufikia nafasi nzuri.

Kilimo kinalipa na kinaweza kubadili maisha ya mtu bila kutegemea ajira kutoka serikalini au kwenye kampuni binafsi.

Wengi waliojaribu kilimo, wameamua kuacha ajira na kujikita kwenye sekta hiyo kwa sababu wameona manufaa yake.

Kilimo cha matunda ni kati ya kilimo kilichobadili maisha ya wakulima wengi. Mathalani, matunda aina ya parachichi yamekuwa na soko kubwa ndani na nje ya nchi na kusababisha wafanyabiashara wengi kutoka nje ya nchi kwa mfano nchi jirani ya Kenya na Afrika Kusini kuja kuyafuata matunda hayo nchini moja kwa moja.

Kilimo cha maua pia kimetoa fursa kubwa ya soko la nje ya nchi na kubadili maisha ya wakulima wengi wa kilimo hicho. Hivi sasa, maua yana soko kubwa kutokana na kutumika kwenye mapambo ya sherehe mbalimbali, kwenye upambaji wa mikutano, ofisini na kwenye misiba.

Kina mama wengi wanamiliki mashamba ya maua na kufungua kampuni zao na sasa wanaishi maisha mazuri bila kutegemea waume zao au ajira.


Pia, wamesaidia kutoa ajira kwa watu wengine kwa kuyaongezea thamani hasa kutengeneza mashada yanayotumika kupamba kwenye sherehe mbalimbali.

Kilimo na ufugaji vimebadili maisha ya wengi na sasa wanaishi bila kupata mawazo ya wapi watapata pesa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Machinga Mbezi Mwisho wangepangwa upya

Na Sabato Kasika

**SEHEMU** kubwa ya eneo la kituo cha mabasi au stendi ya daladala Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, imevamiwa kwa nguvu mpya na wamachinga.

Licha ya eneo lote la Mbezi mwisho sasa kujaa vibanda vilivyofunikwa na nailoni, kilio zaidi kipo upande wa chini wa stendi ya mabasi ya kwenda Kinyerezi, Gongo la Mboto na Temeke.

Hapo wafanyabiashara wadogo na wachuuzi wa kila bidhaa wamerundikana kila upande.

Machinga hao wameweka vibanda kando ya barabara hadi kuziba njia ya wanaotembea , kitendo kinachowalazimisha watumiaji wa njia hiyo wapite barabarani wakipigana vikumbuko na magari, pikipiki na bajaji.

Wengine wameweka vibanda juu ya mitaro ya maji ya mvua. Yaani kwa ujumla mazingira wanayofanyia biashara si rafiki bali ni hatari kwao kama hazitachukuliwa hatua za kuwapanga upya.

Kuna haja ya kuchukua hatua kwa sababu ikitokea ajali wanaweza kupoteza maisha na wengine wengi kujeruhiwa au kuumizwa vibaya, kwani mazingira waliyomo hayawafanyi kuwa na tahadhari dhidi ya hatari yoyote.

Wamo katika vibanda vilivyo juu ya mitaro vikiwa vimezibwa na karatasi za nailoni, hivyo wakiwa ndani hawawezi kuona kinachoendelea barabarani, kwa maana hiyo ikitokea ajali, ni rahisi kuwaumiza.

Ukweli ni kwamba mazingira kama hayo, si vyema watu kukaa na kujisahau kama wako nyumbani huku wengine wakielekeza migongo barabarani kana kwamba wapo katika mazingira salama kumbe ni barabarani.

Ukweli ajali haina kinga, lakini kuchukua tahadhari ni jambo la muhimu, kwani ikitokea ajali eneo hilo watu wengi wanaweza kuumia, na huenda lawama zitaelekezwa serikalini na kumbe chanzo watu wenyewe.

Hatua zinazoendelea sasa za kuwapanga upya machinga wa Kariakoo, zingefika hata Mbezi Mwisho, ili kuwaepusha na ajali zinayowanyemelea, ingawa wao wanaweza kudhani kuwa wako salama.

Barabara nyingi za eneo hilo ni nyembamba, magari yanapishana kwa tabu, huku madereva wa bajaji na bodaboda nao kama kawaida wakiendesha bila kuzingatia sheria ya usalama barabarani.

Katika mazingira hayo, madereva wa mgari wanaweza kuwakwepa na kujikuta wamevamia mabanda ya machinga na kusababisha wafanyabiashara waliomo kwenye maeneo hayo kupoteza maisha.

Ikumbukwe, ni rahisi kwao kugongwa, kwasababu wanapokuwa katika mabanda hayo, hawaoni kinachoendelea barabarani, kwa hiyo hata gari likiacha njia na kuwafuata, hawawezi kujua.

Wakati machinga wakiwa katika hatari hiyo, wapo pia wengine eneo hilo, wanaonyemelewa na janga la kugongwa na magari. Hawa ni wale ambao wanavuka Barabara ya Morogoro bila kufuata utaratibu.

Pembeni mwa barabara hiyo, umewekwa uzio ili wapita njia daraja kuvuka upande wa pili, lakini kuna watu hawatumii daraja, badala yake wanapenya katika uzio, kitendo ambacho ni hatari kwao.

Uzio huo umewekwa baada ya barabara hiyo kupanuliwa, ili kuepusha watu kugongwa na magari, lakini wapo baadhi ya watu wasiotaka kufuata hatua zilizochukuliwa na serikali za kuwanusuru dhidi ya ajali.

Kwa hali ilivyo sasa, nikumbushe kuwa ipo haja kwa mamlaka za manispaa, mkoa na za usimamizi wa barabara kuwasaidia watu wa aina hiyo kuacha mazoea hayo na kuzingatia taratibu, kanuni na sheria kuliko kila mtu kufanya anavyojisikia.

Yote hayo ni kuishi kwa mazoea ambayo yanasababisha watu kufanya lolote wanalojisikia, ikiwamo hata kufanya biashara katika maeneo yenye matangazo yanayowataka wasiwepo eneo husika.

Mtindo huo wa 'kuchezea' mazingira hatarishi, uepukwe ili kuwa katika mazingira salama, kuliko kuendelea kuhatarisha maisha yao bila sababu ya msingi.

Inasikitisha kuona daraja la waenda kwa miguu lipo, lakini watu wanavuka barabara kwa kulazimisha kupenya kwenye uzio, ambao umewekwa ikiashiria kuwa kuna njia ya kuvuka eneo husika.

HABARI KITAIFA

# H'shauri Chalinze yajipanga kukarabati kituo cha afya

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Ramadhani Poss, amesema halmashauri hiyo inatarajia kufanya ukarabati wa Kituo cha Afya Lugoba ambacho kimejengwa zaidi ya miaka 40 iliyopita.

Kadhalika, amesema halmashauri itapeleka gari la wagonjwa katika kituo hicho kurahisisha usafiri kwa wagonjwa wenye uhitaji na wanaopata rufani.

Alibainisha hayo juzi alipokuwa katika kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo na Diwani wa Lugoba alisema kuhusu ukosefu wa gari la wagonjwa katika kituo hicho cha muda mrefu.

Poss alisema tayari halmashauri hiyo ina magari matano ya wagonjwa na suala la ukosefu wa gari kituoni hapo limeshafanyiwa kazi na muda mfupi tatizo hilo litakwisha na pia litatumika katika Kituo cha Afya Msata na Kiwangwa.

"Mbali ya gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Lugoba gari pia tunatarajia kufanya ukarabati katika kituo hicho," alisema.

Diwani wa Bwilingu, Nassa Karama aliomba halmashauri kufikiria upya kupunguza fedha kwa ajili ya tozo ya vizimba na malipo ya taka na maji katika soko jipya jambo ambalo wafanyabiashara wamelalamikia.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo alisema kwakuwa michango hiyo ilipitishwa na madiwani watajadiliana namna ya kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara kuondoa malalamiko yaliyopo.

Mwinyikondo pia amezitaka taasisi zinazofanya kazi katika halmashauri hiyo kuhakikisha zinafanya mikutano na wananchi kwa kuwashirikisha madiwani, ili kusikia kero za wananchi na kuzifanyia kazi kwa kutenga bajeti tatuzi.



Kokoto zikiwa zimewekwa katikati ya barabara ya kwenda Msumi, eneo la Mbezi Makabe, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami. **PICHA: SABATO KASIKA**

# DAWASA yajivunia kuongezeka uzalishaji

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mzingira Dar es Salaam (DAWASA), imesema uwezo wa uzalishaji maji umeongezeka kutoka lita 520,000,000 kwa siku mpaka lita 534,600,000 sawa na ongezeko la lita 14,600,000.

Kauli hiyo imetolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire, katika mwendelezo wa vikao kazi na wahariri wa vyombo vya habari.

Mhandisi Bwire alisema mbali na mafanikio hayo pia, uwezo wa kuhifadhi maji umeongezeka kutoka lita 153,649,000 hadi 183,649,000 sawa na ongezeko la lita 30,000,000, huku mtandao wa usafirishaji na usambazaji maji ukiongezeka kutoka kilomita 4,690.7 hadi 7,087 sawa na ongezeko la kilomita 2,396.3. "Mtandao wa majitaka umeongezeka kutoka kilomita 450 hadi kilomita 517.12 sawa na ongezeko la kilomita 67.12, idadi ya maunganisho ya wateja wa majisafi imeongezeka kutoka 343,019 hadi 438,177 sawa na ongezeko la wateja 95,158," alisema Mhandisi Bwire.

Hata hivyo, DAWASA imeeleza kuwa inadai takribani Sh. bilioni 40 za ankara ya maji kwa wateja mbalimbali.

Mhandisi Bwire alisema madeni hayo yamegawanyika katika maeneo matatu: Taasisi mbalimbali, deni ni takribani bilioni 22, wateja walioondolewa huduma, madeni ni takribani Sh. milioni 15, wateja wa nyumbani, wanadaiwa Sh. bilioni 10. lakini Mhadisi Bwire alisema kuwa bado wanapata maji kwa kuwa madeni hayo ni vumilivu.

Aidha, alisema DAWASA inategemea Mto Ruvu kama chanzo kikuu cha maji na wanapata asilimia 87 ya maji wanayozalisha katika mto huo. Alivitaja vyanzo vingine kuwa ni visima asilimia saba, Mto Kizinga asilimia mbili na Mto Wami asilimia nne.

> **"Mbali ya gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Lugoba gari pia tunatarajia kufanya ukarabati katika kituo hicho," alisema.**

Alisema bado kuna jitihada kubwa zinazoendelea ili kuhakikisha mtandao wa kilomita 7,087 unaohudumiwa na mamlaka hiyo mkoani Dar es Salaam na Pwani unakuwa na ufanisi mkubwa na kuleta matokeo chanya kwa wananchi na mamlaka kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Mhandisi Bwire; licha ya kutoa huduma mkoani humo pia DAWASA inatoa huduma katika baadhi ya maeneo mikoa ya Tanga na Morogoro.

"Katika kuboresha maeneo yetu ya huduma tumegawa mikoa ya kihuduma ya DAWASA takribani 23. Ilani inatutaka ifikapo 2025 tuwe tumefikia asilimia 95 ya huduma ya maji, lakini kwa sasa kwa mwelekeo wamefikia asilimia 93 kutokana na mtandao wa usambazaji maji. Kazi kubwa tuliyo nayo ni kuangalia ni kwa namna gani haya maji yanawafikia wananchi." alisema Mhandisi Bwire. Alisisitiza kuwa kuna maeneo ambayo yanapata maji muda wote, mengine kwa mgao huku maeneo mengine yakiwa katika hatua ya kufikisha huduma ya maji, ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

"Ukienda maeneo ya Kigamboni kuna maji ya kutosha, kinachotakiwa ni kuongeza mtandao wa usambazaji vivyo hivyo kule Mkuranga na kwingineko."

Mhandisi Bwire alisema kuwa kutokana na vyanzo vya maji vilivyopo kuonekana kuelemewa wapo mbioni kupata vyanzo vingine vya maji ikiwamo kutoka Mto Rufiji na Bwawa la Kidunda.

Akizungumzia Bwawa la Kidunda, alisema lengo la ujenzi wake ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi kwa kuhakikisha maji katika Mto Ruvu yanapatikana kwa kipindi chote cha mwaka ili kutoa huduma ya majisafi kwa mikoa ya Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo.

Alisema kuwa mradi huo ukikamilika utawezesha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa matumizi ya majumbani na viwandani, kwa ufanisimkubwa pamoja na nishati ya umeme na baadaye kuangalia namna ambavyo litasaidia katika kilimo cha umwagiliaji.

Ujenzi wa bwawa hilo ambao unatekelezwa na serikali ya awamu ya sita unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 300 na Mkandarasi ni Sino Hydro Corporation kutoka China ambaye tayari ameanza utekelezaji wake. Aidha, kukamilika Mradi wa Kidunda utawezesha mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini yenye kuzalisha jumla ya lita milioni 466 kwa siku, kuwa na uwezo wa kuzalisha maji katika majira yote ya mwaka na hivyo kuepusha upungufu wa maji katika majira ya kiangazi nchini.

HABARI PICHANI

# MAONESHO YA WAKULIMA NANENANE KATIKA PICHA



Mkulima wa matunda kutoka Kata ya Songa, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Richard Ismail (kushoto), akiwauzia machungwa wateja waliotembelea banda la Muheza katika Maonesho ya Wakulima Nanenane, mkoani Morogoro juzi, ambapo ameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kujenga kiwanda kidogo cha kusindika matunda ili kuondoa changamoto ya ukosefu wa soko kwa wakulima hao. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge (mwenye skafu), akipata maelezo alipotembelea banda la Tigo, katika Maonesho ya Wakulima Nanenane, mkoani Morogoro, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Luteni Makame Makame, alipotembelea banda la Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), katika Maonesho ya Wakulima ya Nane Nane katika Viwanja vya Dole, Zanzibar jana. **PICHA: OMPR**



Bwana shamba wa kampuni ya mbegu ya SEEDCO, Afrey Maziko (kulia), akitoa maelezo kuhusu mbegu mbalimbali za mazao kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni (kushoto) na wananchi wengine, waliotembelea Maonesho ya Wakulima Nanenane ya Kanda ya Kaskazini, Njiro jijini Arusha, jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Wakala wa Airtel Tanzania, Antony Kumwenda (kushoto), akitoa maelezo kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na kampuni hiyo kwa watu waliotembelea Maonesho ya Wakulima Nanenane, Nyakabindi, wilayani Bariadi, mkoani Simiyu juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**





# Upanuzi Bandari ya Tanga waanza kulipa

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MENEJA Mkuu wa Uwakala wa Meli wa Sea Front Shipping Service (SSS), Neelakandan CJ amesema Bandari ya Tanga katika mwezi huu inatarajia kupokea meli kubwa za mizigo mchanganyiko tatu hadi nne.

Alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mapokezi ya Meli ya Mv. Annegriti.

Meli hiyo ilikuwa na shehena ya mizigo mchanganyiko, inayokadiriwa kuwa na uzito wa tani 14,000 ikitokea China.

Alisema ujio wa meli hiyo umeweka alama ya kipekee kwa kuwa haijawahi kutokea meli ya mizigo mchanganyiko kushusha kiwango kikubwa cha mzigo zaidi ya magari 500 na mizigo mingineyo.

"Baadhi ya mizigo itaelekea katika nchi za jirani ikiwamo Zambia, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Malawi na Rwanda, pia mizigo mingine itabaki hapa nchini," alisema.

Aidha alisema kutokana na umuhimu wa bandari hiyo kwa maendeleo ya nchi wanatarajia kupokea aina nyingi ya mizigo kuelekea nchi za jirani. Alisema hatua hiyo itasaidia wafanyabiashara na watoa huduma za usafiri wakiwemo mawakala wa forodha na wananchi kwa pamoja kunufaika kutokana na ujio wa meli zitakazokuwa zinatia nanga katika bandari hiyo.

**"Kuja kwa meli hii ni matunda ya uwekezaji ambayo yamefanywa na serikali kwa kuwa kumefanyika uwekezaji wa Sh. bilioni 429 kuiboresha ya bandari na sasa...**

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, akizungumzia ujio wa meli hiyo alisema ni juhudi zilizofanywa na serikali katika kuboresha bandari hiyo, kwamba Sh.bilioni 429 zilitumika kwenye uboreshaji huo

Alisema uwekezaji huo umekuwa ni chachu ya kuifungua bandari, huku akitoa rai kwa wadau kutumia Bandari ya Tanga, kwa ajili ya kusafirisha mizigo na kuleta meli za abiria kwa kuwa maboresho yamefanyika kwa kiwango cha juu.

"Kuja kwa meli hii ni matunda ya uwekezaji ambayo yamefanywa na serikali kwa kuwa kumefanyika uwekezaji wa Sh. bilioni 429 kuiboresha ya bandari hadi sasa tumeshuhudia meli kubwa kutoka China ikifika hapa, ikiwa imetumia siku 21, hadi kutia nanga ikibeba magari 500," alisema Kihenzile.

Vilevile, alisema uwekezaji wa fedha hizo umesaidia kuongeza kina kutoka mita tatu mpaka 13 kwa kuwa awali meli hiyo isingeweza kutia nanga, kwamba kulifanyika upanuzi na eneo la kuingilia na kutokea meli kwa takribani upana wa mita 73.

Kihenzile alisema fedha hizo zilisaidia kuongeza eneo la kugeuzia meli kwenye kipenyo cha takribani mita 800.



Ofisa madini mkazi Mirerani, Nchagwa Marwa Chacha (kushoto), akizungumza kuhusu mikakati ya kuboresha uchimbaji madini ya Tanzanite, wakati wa kikao cha wajumbe wa eneo tengefu la Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara juzi. Katikati ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Fakii Lulandala. **PICHA: GIFT THADEY**

# Naibu Waziri awapa somo wafugaji nyuki

**Na Mwandishi Wetu,** KOROGWE

WAKATI Tanzania ikitarajia kuwa mwenyeji wa mkutano wa dunia wa ufugaji nyuki, wadau wametakiwa kuichukulia sekta hiyo kwa uzito mkubwa kwa kuimarisha ili kuvutia wawekezaji pamoja na kuongeza tija katika ufugaji huo.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Danstan Kitandula alisema hayo juzi wakati alipofanya ziara ya kutembelea miradi ya ufugaji nyuki, kuangalia shughuli zinazofanywa na wadau wa Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) za kulinda uhifadhi.

Moja ya miradi hiyo ni wa ufugaji nyuki katika Kijiji cha Mkwakwani wilayani Korogwe mkoani Tanga, ambapo ni moja ya vijiji vilivyopatiwa mradi huo ili kupunguza kasi ya uvunaji wa misitu kwa ajili ya kuni na mkaa.

Kitandula alisema licha ya nyuki kuwa na mchango mkubwa katika eneo la kuchavusha mazao ya chakula lakini pia ni njia ya kuongeza kipato kwa wafugaji kutokana na mazao yake.

Alisema asali imekuwa na matumizi mengi kama kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwemo sabuni na kuifanya iwe na soko kubwa ndani na nje ya nchi.

"Mataifa mbalimbali watashiriki mkutano huo, nitoe rai kwa wahusika wa sekta hii tuichukulie kwa uzito, tukiweka mkazo itatuwezesha kiuchumi na kuwawezesha watu wetu kutoka kwenye umasikini,". Alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa EAMCEF, Francis Sabuni, alisema lengo la mradi huo ni kupunguza uharibifu kwenye misitu ambao ulikuwa ukiharibiwa na shughuli za kibinadamu.

Alisema tangu mwaka 2006, EAMCEF imekuwa ikitoa ruzuku kwa wananchi wanaopakana na hifadhi za mazingira asili zilizopo ndani ya safu za Milima ya Tao la Mashariki, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwashirikisha wananchi kwenye uhifadhi na ulinzi wa bayoanuai hizo.

Vilevile alisema kwa mwaka Mkoa wa Tanga, wenye hifadhi tatu za amani, Magamba na Nilo, mfuko huo umekuwa ukitoa Sh. milioni 600 kila mwaka kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ufugaji nyuki, asali, kilimo cha miche ya viungo, majiko banifu na upandaji miti.

Katibu wa kikundi cha ufugaji nyuki (Kwasamkwa), Walles Singano, alisema maisha yao yameanza kubadilika kwa kuwa wamefanikiwa kuongeza kipato kutokana na uwekezaji katika ufugaji nyuki.

Alisema mapato yatokanayo na asali yameongezeka kutoka Sh.500,000 hadi Sh.milioni 1.6 kwa mwaka 2021 na kwamba walivuna asali lita 160 mwaka 2022 asali lita 115, ambayo waliuza Sh. milioni 1.15.

"Mavuno ya asali yanasababishwa na mabadiliko ya tabia nchi, kwa kuwa mvua ikizidi au ukame ukiwepo kwa muda mrefu hupunguza uzalishaji, tunajitahidi kuendelea kuzingatia ushauri wa wataalama," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, William Mwakilema, alisema uhifadhi ni muhimu na wataendelea kushirikiana na mfuko huo na wadau wengine katika kuhakikisha wanahifadhi mazingira ikiwemo upandaji wa miti na miradi mingine.

# Bil.8/- kupeleka huduma ya maji wachimbaji madini

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WACHIMBAJI wa madini ya tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wanatarajia kuondokana na kero ya maji baada ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA), kuanza utekelezaji wa mradi wa Sh.bilioni 8.3

Mkurugenzi Mtendaji wa AUWSA, Justin Rujomba, alisema hayo jana wakati akizugumza na waandishi wa habari kuhusu mkakati wa kuwapatia maji safi na salama wachimbaji madini hao wa Mirerani.

Rujomba alisema baada ya kupatikana fedha hizo wataanza kuweka miundombinu ya maji kwa kuwa wameshafanya utafiti kupitia wataalamu kisha kusambaza maji.

Alisema hivi sasa wamejipanga kutekeleza agizo la Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala, kufikisha huduma ya maji kwa wachimbaji madini ya tanzanite ndani ya siku saba.

Alisema watafanikisha hayo kupitia mipango miwili ambapo mpango wa muda mfupi watatekeleza kwa kutumia magari na mpango wa muda mrefu watasambaza maji ya bomba.

"Kwenye mpango wa muda mrefu, tunatarajia kutumia fedha hizi na itakuwa suluhisho ya kupatikana kwa maji safi na salama kwenye machimbo ya madini ya tanzanite," alisema Rujomba.

Vilevile alisema kwa mpango wa muda mfupi wataingiza maji kupitia magari yatakayokuwa yamebeba maboza ya lita 10,000 wakitumia bei elekezi ya serikali ambayo imepangwa na (EWURA).

"Magari yatakuwa yanachota maji safi na salama yaliyopo mji mdogo wa Mirerani na kuyaingiza ndani ya ukuta unaozunguka mchimbo kwa kuyamwaga kwenye matangi yaliyopo ndani," alisema.

Pia, alisema baada ya hapo watatimiza mpango wa muda mrefu wa kufikisha maji kwa kuwa wameshafanya utafiti na kusubiria fedha hizo ambazo zitafanikisha miundombinu ya maji.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala, alisema ametoa muda wa siku saba kwa AUWSA, kuhakikisha wachimbaji na watu waliopo ndani ya ukuta wanapata maji.

Alisema: "Tumewaagiza AUWASA, wasambaze maji ndani ya siku saba na baadaye wahakikishe wanafanikisha upatikanaji wa maji safi na salama kupitia bomba".





# Operesheni kamata wakimbizi wakaidi yanukia

**Na Vitus Audax**

SERIKALI inatarajia kufanya operesheni ya kuwabaini wakimbizi katika kambi ya Nyarugusu na Nduta zilizopo mkoani Kigoma ambao wanatoroka na kukwepa kurejea makwao.

Hatua hiyo ni kutekeleza makubaliano ya pande tatu za nchi ya Burundi, Tanzania pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia wakimbizi (UNHCR) kuwa ifikapo Desemba 1, 2024 wakimbizi wawe wamerejea makwao kwa hiari.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo alisema hayo wakati akihitimisha ziara yake na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Maendeleo ya Jamii na Usalama wa Raia wa Burundi Brigedia Jenerali Nibona Bonansize katika kambi za wakimbizi za Nyarugusu na Nduta mkoani hapa.

Sillo alisema serikali itachukua hatua hiyo endapo idadi ya wakimbizi wanaojitokeza kurudi kwao kwa hiari itaendelea kuwa ndogo.

"Urejeaji huu ni wa hiari kama yalivyo makubaliano yetu lakini kama serikali tunatoa wito na tunasisitiza warudi wakaijenge nchi yao ya Burundi ambayo iko salama," alisema Sillo.

Alisema serikali ina mpango mahususi baada ya muda huo kwenda nyumba kwa nyumba kufanya tathimini ya kila mkimbizi kujua tatizo, kwanini amekimbia na kwanini anakuwa na mashaka ya kurudi nchi na wakati nchi iko salama.

"Tutafanya tathimini ya kutosha kwa mtu kwa mtu, familia kwa familia na kuhakikisha tunapata sababu za kutosha kwamba kwanini hawataki kurudi nyumbani. Lakini tunaendelea kuhamasisha kwamba lengo na nia ni kuhakikisha kwamba wanarudi salama nyumbani kwao," aliema Sillo.

Naibu Waziri wa Burundi Brigedia Jenerali, Nibona Bonansize alisema hali ya kiusalama nchini humo ni salama na shughuli za kimaendeleo zinaendelea vyema, hivyo kuwataka raia wa Burundi waliopo katika makambi hayo kurejea nyumbani.

Pia, aliwataka wazazi wote kurejesha watoto wao ili kuhakikisha wanapata elimu na haki zao za msingi, kwamba kuendelea kubaki kambini wanazidi kukosa haki zao za kimsingi.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy (kushoto), akizungumza wakati wa semina ya waandishi wa habari mkoani humo, juzi na kuwataka washirikiane kikamilifu katika kukabiliana na vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Uhaba wa viti hospitalini wawaibua madiwani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuongeza viti kwa ajili ya wagonjwa na watu wanaosubiria huduma wakiwemo wajawazito katika Hospitali ya Halmashauri hiyo.

Wamesema hospitali hiyo inahitaji viti ili kuondoa adha wagonjwa kusubiria huduma wakiwa wamesimama koridini.

Wakielezea tatizo hilo kwa nyakati tofauti katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya nne ya mwaka 2023/24. Baadhi ya madiwa hao akiwemo, Diwani wa Kata ya Mega, Patrick Mazuri alisema kwa sasa wagonjwa wengi wanazagaa ovyo katika mazingira ya hospitali kwa sababu ya ukosefu wa viti, kwamba vilivyopo havikidhi mahitaji ya wingi wa wagonjwa wanaofika kupata huduma. Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira wa baraza la madiwani hilo, Six Masanja ambaye ni Diwani wa Mwakata alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kusema kamati yake inalifanyia kazi ili kuhakikisha wagonjwa wote wanapata sehemu ya kukaa wakati wakisubiria matibabu.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mibako Mabubu alisema hospitali hiyo haina muda mrefu tangu ilipokamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi. Alisema hivyo mapungufu kama hayo ni kawaida kuwepo na kuagiza Ofisi ya Mganga Mkuu kuwasilisha changamoto zote zinazoikabili ili kuangalia namna ya kuzitatua kwa haraka.

# TAKUKURU yatoa tahadhari kuelekea uchaguzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, imewatahadharisha wananchi kuwa makini katika uchaguzi ujao, kwamba wachague viongozi wenye sifa na uwezo wa kuwaletea maendeleo na siyo watoa rushwa.

Tahadhari hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy, wakati wa ufunguzi wa semina kwa waandishi wa habari mkoani hapa iliyohusu nafasi ya vyombo vya habari katika mapambano dhidi ya rushwa. Alisema ni muhimu kwa waandishi wa habari kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kufanya maamuzi sahihi katika kuchagua viongozi makini katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu 2025.

> **"Wagombea watoa rushwa hawawezi kuwaletea maendeleo wananchi, hivyo wanapaswa kuwa makini na kufanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi ...**

Alisema rushwa inatishia demokrasia na kuwanyima wananchi haki yao ya kupata viongozi waadilifu kwa kuendekeza tamaa na fedha za muda mfupi. "Wagombea watoa rushwa hawawezi kuwaletea maendeleo wananchi, hivyo wanapaswa kuwa makini na kufanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi wanaowafaa," alisema Kessy. Pia, aliwataka waandishi wa habari kuzingatia maadili ya taaluma zao kipindi cha uchaguzi na kuepuka kutumiwa na baadhi ya wanasiasa ambao watawapatia rushwa.

Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Doo, alisema lengo la kuzuia vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi ni kuwa na viongozi wazalendo wenye kuchukia rushwa katika nchi yao.

# Wakulima watolewa hofu usambazaji pembejeo

**Na Halima Ikunji,** TABORA

KAMPUNI ya Mbolea Tanzania (TFC) imewataka wakulima kuanza maandalizi ya msimu mpya wa kilimo mapema, huku ikiwahakikisha kuwa mbolea itakayosambazwa ni yenye ubora na viwango sahihi na itawafikia kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu wa TFC, Samwel Mshote alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe katika maonesho ya Nane nane Ipuli mkoani hapa.

Alisema serikali imefanya jitihada zote ili kuhakikisha mbolea ya ruzuku itakayosambazwa kwa wakulima msimu huu inakidhi viwango vyote vinavyotakiwa ili kuwezesha wakulima wa mikoa yote kufanya kilimo chenye tija.

Mshote alisema utaratibu wote wa uagizaji na kuthibitishwa ubora wa pembejeo husika umeshafanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), hivyo akawatoa hofu wakulima kuhusiana na ubora wa pembejeo msimu huu.

Alisema msimu uliopita waliagiza na kusambaza mbolea katika mikoa yote kwa wakati vivyo hivyo kwa mwaka huu hawatawaangusha wakulima, watahakikisha mikoa yote 26 inafikishiwa kwa wakati.

Aidha alisema, wataendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wote ili kufanya shughuli zao kwa weledi na kwa matokeo chanya.

Baadhi ya wakulima akiwemo John Yamungu kutoka Wilaya ya Uyui waliishauri serikali kuhakikisha inaweka utaratibu maalum utakaosaidia mbolea hiyo kuwafikia wananchi waishio maeneo ya pembezoni kwa wakati ili waanzishe kilimo mapema.



Ukurasa 12

KUTOKA VIWANJA VYA NANENANE

**TALIRI yaja na teknolojia mpya yenye mapinduzi mbegu za mifugo**




Ukurasa 13

Michoro ya miguu ya panzi haijatusaidia

BUFE

IJUMAA AGOST 9, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**Wanawake Tabora walivyojitosa kwenye mapori kufuga nyuki**

BIASHARA

# Haya ni machache usiyoyajua ndani ya treni ya umeme 'SGR'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SI ajabu kuishi Dar es Salaam na kufanya kazi Morogoro. Ni kutokana na kutimia kwa ndoto ya usafiri wa mwendokasi wa treni ya umeme inayotembea kwa kasi ya kilometa 160 kwa saa.

Inahitaji takribani dakika 90 kufika stesheni ya Morogoro na kuingia ofisini kwake bila uchovu, kuchafuka wala kuchelewa kazini.

Pamoja na hayo, yapo mengi yanayovutia kuutumia usafiri huo. Mosi, ndani ya mabehewa kuna wahudumu waliopewa mafunzo maalumu kama wale wa kwenye ndege (cabin crews).

Hawa wana majukumu mengi kama vile kuwapa taarifa muhimu na maelekezo wasafiri ndani ya treni hiyo inayotumia umeme, kuwapa chakula na vinywaji wasafiri.

Uwapo ndani ya treni hiyo, mawasiliano hufanyika kwa lugha kuu mbili nazo ni Kiingereza na Kiswahili, kuwasiliana na abiria katika kila hatua ya safari ikiwamo taarifa za stesheni au vituo wanavyoingia.

Ni usafiri usio na bughudha kwani hakuna kutikisika wala kurushwarushwa, hivyo abiria hunywa vinywaji kwa utulivu bila kutikisika. Ina mengine mengi kama msafiri huyu aliyetoka Dar kwenda Dodoma anavyosema:"

"Hii ni ndege ya ardhini napenda kuita hivyo, kwa sababu utaratibu wake wa kufika stesheni ni saa mbili kabla ya kupanda treni, hivyo unashabihiana na wa ndege. Lakini ukiacha hilo muda unaotumia kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam



Rais Samia Suluhu Hassan.

unazidi ndege kwa saa 2:35 hivi, tunashukuru serikali hakika historia imeandikwa Tanzania,"

Ni Beatrice John, mkazi wa Dodoma na mmoja wa wasafiri wanaopanda treni hiyo. Anafurahi kupanda usafiri huo huku akiufananisha na ndege kwa kuokoa muda.

"Hii treni ni raha, hufungui mlango wala dirisha, ukiingia agana na ndugu zako chini kama ilivyo kwenye ndege huwezi kufungua dirisha wala kupunga mkono. Jamani hakuna kuweka mabegi chini ya siti kama kwenye basi."

"Tumeondokana na kusota barabarani siku nzima, kwa sasa kwani nina uhakika wa kuondoka asubuhi kwenda kununua bidhaa zangu Kariakoo nikafunga mzigo na nikapakia kwenye magari ya mizigo nikarudi Dodoma jioni bila kulala tena Dar es Salaam,"anasema.

Anasema kwanza kwa safari za treni hiyo ni mkombozi kwao hasa wafanyabiashara hata wafanyakazi kwani imeokoa gharama za maisha.

Mfanyabiashara Carlos Mrema, anaeleza kuwa treni hiyo inaunganisha jiji kuu la kibiashara la Dar es Salaam na Dodoma ambapo ni makao makuu ya serikali, hivyo itaongeza unafuu wa baadhi ya bidhaa kwa wananchi.

"Hii treni inatuhusu sote, kwa mfano kuna watu wa mikoa ya kanda ya ziwa wanaipandia Dodoma wakielekea Dar es Salaam hivyo pia inasaidia kuokoa muda kwani wasafiri hawa wanafika mapema kuliko ilivyokuwa ambapo walikuwa wanafika usiku wa manane,"anasema.

Anaeleza kuwa, uchumi wa wafanyabiashara wa Dodoma utakua kwa kiwango kikubwa kutokana na SGR kuchochea mzunguko wa biashara.

"Sisi wafanyabishara mzigo ulikuwa unachukua siku mbili hadi tatu kufika lakini kwa sasa unapanda treni, unakwenda kununua, unarudi na unapokea mzigo wako,"anasema.

Mkazi wa Dodoma, Abdulrahman Fumo, anaisifu serikali kwa kukamilisha kazi ambayo ilianzwa na serikali ya awamu ya tano.

"Ninajivunia kwa kweli uchumi utakua maana mtu atasafiri kwa saa tatu kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, mwitikio wa kutumia SGR ni mkubwa, uchumi utapaa," anasema.

Dereva bodaboda katika stesheni ya Mkonze, Ali Hassan, anasema ni moja ya mradi utakaowaongezea kipato kwa kuwa watawasafirisha abiria wa SGR na mizigo yao wanaoshuka kwenye stesheni hiyo.

"Wananchi tumenufaika na mradi huu tumepata ajira kama kufanya usafi, kukata tiketi, pia mradi umefungua fursa nyingi kwetu tunaishukuru serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza jukumu hili,"anasema.


Akizindua safari za treni hiyo, Rais Samia, anasema mradi wa SGR siyo ndoto tena au kitu cha kufikirika kwani uhalisia umeonekana na watu wanatumia kama ambavyo waliwaza hapo awali. Anawataka Watanzania kuongeza chachu ya kufanya kazi kwa sababu treni hiyo ni ushahidi kuwa 'tunaweza'.

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

KUTOKA VIWANJA VYA NANENANE

# TALIRI yaja na teknolojia mpya yenye mapinduzi mbegu za mifugo



Mbuzi chotara wanaotokana na kuchanganya mbegu za asili na jamii kubwa kutoka nje ya nchi. Malisho ya kisasa ya mifugo. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

**Na Neema Emmanuel,** DODOMA

MAADHIMISHO ya Siku ya Wakulima Nane Nane Kanda ya Ziwa Magharibi mwaka huu ni ukurasa mpya. Yamekuja na utaalamu wa kuboresha mifugo hasa ng'ombe na mbuzi wafugike katika mazingira magumu.

Teknolojia hiyo inawawezesha wanyama hao kustahimili mazingira ya malisho haba na upungufu wa maji, bila kuathiri uzalishaji wa maziwa na nyama.

Hiyo inakuja kupiku uhalisia uliopo maeneo mengi ya Kanda ya Ziwa kwenye ufugaji mkubwa wa ng'ombe wa nyama na uzalishaji, hata kuwa fursa mpya kwa wafugaji hao.

Siri iliyoko ni fursa ya kutumia madume bora na mbegu za kisasa kufanya mabadiliko ya kuingia kwenye ushindani wa soko. Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI )Kanda ya Ziwa, Kituo cha Mabuki, Dk.Heriel Massawe, anasema mwitikio wa wafugaji kutumia teknolojia hiyo umeongezeka maradufu.

Anafafanua kuwa, hilo limekuwa likiendana na usambazaji madume bora, kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wanufaika na kufuatilia matunzo na hali ya kukua kwa ufasaha.

Mtaalamu huyo anaeleza kuwa,taasisi hiyo ya Kanda ya Ziwa ina jukumu la kutafiti mifugo, hususani aina ya ng'ombe, mbuzi na kondoo, ili kuakisi minyonyoro ya thamani na kuiendeleza sekta ya mifugo.

> **"Wa mwaka mmoja unaweza kudhani ana miaka miwili, hii ni tofauti na ufugaji wa asili. Ili kufikia 'dau' nililopewa, lazima niuze ng'ombe wawili hadi watatu hawa wa kawaida...**



Hapo anataja wanajikita katika mikoa sita ya kanda hiyo, wakiwafunda wafugaji utaalamu wa teknolojia hiyo ya uzalishaji na utunzaji malisho, ili waondokane na ufugaji wa kienyeji, badala yake wahamie kwenye wa kisasa wa kutumia madume bora ya mifugo, kuboresha maisha yao kiuchumi.

"Changamoto tuliyonayo tunatakiwa kufanya kazi kwa bidii, ili tuzalishe mazao mengi tumezidiwa na wateja wanazitaka kwa wingi lakini tunafikia wakati tunakuwa hatuna njia ya kutatua tatizo.

"Hili linatupasa tufanye kazi kwa bidii na ubunifu, ili kuwatosheleza wafugaji, pia watambue kuwa bila malisho hakuna ufugaji lazima uwe na majani ndiyo ufikirie kufuga kwa sababu majani ndicho kitu muhimu, " anaeleza.

Anawatafsiri wafugaji kwa nafasi yao, ni watu muhimu kwa sababu ndio wanazalisha nyama inayoingia sokoni na kulisha watu wote, japo bado wako katika stadi za kijadi.

Hapo ndiyo nafasi yao TALRI, wakijikita kutoa elimu, sambamba na kugawa mbegu, pia ng'ombe aina ya ankole wenye pembe ndefu, akiwataja ni wanyama wenye ubora mkubwa, pia ladha sahihi kwa mlaji.

Anasema wakiwa kituoni kwao, huwa wanazalisha mbegu na wanyama hao wakati wote wakiwa chini ya tathimini zao tangu wanazaliwa, wanapoachishwa na wanapotimiza umri mwaka mmoja, wanachukuliwa uzito.

Dk. Massawe anasema, baada ya hatua hiyo kuna vitu anavyovitaja kuwa ni vigezo vya kuchagua ambao wapo juu katika anachokitaja ni kiwango cha kitaalamu asilimia 60, kwamba wanakuwa na ubora wa kusambazwa kwa wafugaji kama mbegu.

### TEKNOLOJIA YA NG'OMBE

James Manjala ni mmoja wa wafugaji walionufaika na teknolojia hiyo, anaeleza kuwa alianza ufugaji ng'ombe wa asili kwa kutumia dume aina ya ankole na mara baada ya kupewa elimu ALIRI- Mabuki, baada ya hapo wakafanya uamuzi kuchukua dume aina hiyo, akikiri sasa limewaletea mabadiliko makubwa, hata kuboresha maisha yao.

Anaeleza kuwa mchanganyiko wa ankole na ng'ombe wa kienyeji unakuwa haraka', akisema unachangia kurahisisha soko, tofauti na awali walivyojikita katika ufugaji asili. Ndani ya hiyo, mfugaji huyo anataja kunufaika na ongezeko la maziwa, akiwa na ufafanuzi: " Nikienda mnadani mifugo yangu inakimbiliwa inavutia, ina uzito mkubwa nauza kwa bei ninayoitaka mimi."

Anaendelea: "Wa mwaka mmoja unaweza kudhani ana miaka miwili, hii ni tofauti na ufugaji wa asili. Ili kufikia 'dau' nililopewa, lazima niuze ng'ombe wawili hadi watatu hawa wa kawaida..."

Mfugaji wa ngo'mbe aina ya Mpwapwa, Mathayo Reuben anaieleza aina hiyo ni zao la mchanganyiko wa vinasaba vya ng'ombe kutoka Ulaya,Asia na wa Tanzania.

Anaeleza kwamba, ameamua kutumia teknolojia hiyo kujiongezea kiwango cha lishe, pia mapato, ng'ombe huyo hutoa maziwa lita sita hadi nane kwa siku.

### TEKNOLOJIA YA MBUZI

Akizungumzia teknolojia hiyo, Amos Jisoli, Ofisa Mifugo Mwandamizi wa TALIRI, anaeleza walivyoamua kuboresha ufugaji mbuzi wa asili, kwa kutumia madume bora anayoita 'Malya' kupata nyama bora inayoleta ushindani sokoni.

Jisoli anasema mbuzi hao kuanzia uzao wa pili wanauwezo wa kutoa mapacha, tenawanaokuwa haraka na wenye uzito mkubwa .

Anaeleza TALIRI wanajamii tatu akizitaja kuwa ni mbuzi Boar, Malya na chotara wa Boar wa kienyeji, hivyo wanawatumia kuwashauri wafugaji kutumia madume na mbegu bora, kubadilisha aina za mifugo yao majumbani, wengi wakiwa wenye mbegu duni zinazowachelewesha kuingia sokoni

"Boar ameletwa kwa mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lengo ni kuboresha mbari za wafugaji.Mfano, teknolojia yetu mbuzi jike anazaliwa akiwa na kilo 1.8, lakini dume akizaliwa ana kilo 2 5.

"Baada ya miezi mitano jike anafikia kilo 7.9 wakati dume ni kilo 8.7 pia watoto wanastahimili mazingira. Lakini pia kuna jike ambalo limezaliwa kienyeji baba na mama asili yao ni kienyeji alikuwa na kilo 1.6 lakini baada ya miezi mitano alikuwa na kilo 4.2 kuna tofauti kubwa sana karibia mara mbili na chotara," anaeleza Jisoli.

Mfugaji anayejitambulisha, Mzee Nyanda, anaunga mkono akitoa hamasa kwa wafugaji wenzake waondokane na mfumo wa kienyeji, badala yake wajikite madume bora ya mifugo.

" Tulipewa elimu ya kutosha mbuzi huyu anauwezo wa kuhimili magonjwa ya mifugo ,kiwango kikubwa cha utoaji maziwa na nyama, mbuzi huyu anatokana na mchanganyiko wa mbuzi wa kienyeji kwa asilimia 15 .

"Mbegu hii tumeambiwa inatokea Pakistan na Boer asilimia 30 kutoka Afrika ya Kusini ukweli sijutii kutumia teknolojia hii yenye gharama nafuu" anaeleza, huku akionyesha mifugo yake.

### CHANGAMOTO MALISHO

Kwa ujumla TALIRI Mabuki inasema kuwa kiuchumi, asilimia 70 ya wananchi wanategemea kilimo na mifugo, huku mifugo ikichangia asilimia saba ya pato la taifa.

Inasema, licha ya kuchangia pato hilo inakabiliwa na matatizo mengi yakiwamo magonjwa, maji,maeneo ya malisho na kukosa mbegu bora za malisho ya wanyama.

Kwa mujibu wa TALIRI teknolojia hiyo ya kisasa ni mkombozi kwa wafugaji, kwani inatoa urahisi katika gharama za kuwahudumia. Aina tano za mbegu za majani zilizopata ithibati ya kusajiliwa na Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) huku mzalishaji akiwa taasisi hiyo ni pamoja na Macroptilium Altropurperium(Siratro); Cenchrus Ciliaris (Buffel Grass), Chloris Gayana (Rhodes Grass); Medicago Sativa (Alfalfa); na Desmodium Intortum.

Teknolojia hiyo imepunguza uhaba wa malisho, ununuzi wa mashudu ya alizeti au vyakula, pia inaongeza protini kwa afya ya wanyama, ikimnufaisha mfugaji kwa kuongeza kipato.

Juma Elias ni mdau anayezungumza na Nipashe,akieleza kuwa taasisi hiyo ipo takribani miaka 60 iliyopita ya uzalishaji wa mifugo wamefanya kazi nzuri ya kisayansi kuondoa mapengo ya kitaalamu katika uzalashaji mbegu hizo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Michoro ya miguu ya panzi haijatusaidia






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

WAAFRIKA tukiwamo Watanzania, baada ya kupata uhuru na kutamba kumfukuza Mkoloni, tulijikita katika kujenga upya nchi yetu huku tukipambana na maadui waliosalia; ujinga, umasikini na maradhi.

Katika kukabiliana na ujinga, tukajenga shule zetu wenyewe na kuhakikisha kuwa tunafundisha wanetu kupambana nao, lakini tukiwapanga kujiletea maendeleo katika nchi hii changa.

Tukawafundisha historia ya Malkia Elizabeth na kuwaambia ni kwa nini tuna Ziwa Victoria na si Ziwa Nyanza, ili mradi tuwakumbushe ya Wazungu waliotutawala.

Wakafundishwa jinsi David Livingstone alivyokuja nchini mpaka akafika Ujiji, Kigoma na jinsi William Speke alivyogundua Mlima Kilimanjaro kana kwamba katika maeneo uliko Mlima huo, hakukuwa na watu.

Tukataka kuandaa madaktari wetu ndipo tukawafundisha somo la Sayansi, kwa kuwataka wachore panzi na kuonesha miguu yao na jinsi wanavyoitumia kujitafutia chakula.

Tukawaambia kuwa, hata nzi ana macho mengi kama milioni hivi na hivyo ana uwezo wa kuona vitu vingi kwa wakati mmoja, tukiwahimiza kumchora nzi, panzi na mende na kuonesha sehemu za miili yao.

Mwanafunzi aliyechora vizuri akaonekana shujaa darasani na hata kupewa cheo cha kuongoza wenzake, kwamba ndiye kichwa cha darasa kwa kuweza kumchora nzi au panzi vizuri.

Hata sekondari tukawafundiasha somo la Biolojia na kuwapasulisha vyura na panya, ili waje kuwa madaktari wa binadamu. Hebu fikiria wapi na wapi binadamu na chura!

Fikiria hayo maelfu ya macho ya nzi yatalisaidia nini Taifa hili masikini linalotafuta maendeleo ya kiuchumi? Tukasonga mbele na kufundishana Kiingereza na aliyeweza kukimumunya vizuri, akaonekana ndiye msomi.

Na hata majina ya jadi yakaepukwa na kupachikwa ya Kizungu, ili kuonekana wasomi na ndiyo sababu hata shule za Kiingereza zikaitwa za kimataifa kwa asomaye huko, ndiye hasa mtaalamu kuliko wa senti Kayumba.

Watoto wakapoteza miaka na miaka shuleni kujifunza kuchora panzi na kupasua panya na kutambua sehemu za miili ya mende na vinyonga, na baadaye kurudi mitaani bila jambo la kufanya na kujikuta wakitakiwa kujiajiri.

Hebu tufikirie, hivi leo hii mtoto aliyesomea kuchora panzi na mende ana nafasi gani katika jamii hii ya kidijitali? Shule zilizokuwa za ufundi tukaona zinatupotezea muda na kuzibadili kuwa vyuo vikuu na kuzalisha wataalamu wa nadharia.

Tukaibua na mtazamo wa kuajiri watu kwa kuangalia vyeti hata kama kichwani hamna kitu, lakini kwa kuwa na vyeti tu ni sifa ya kupata ajira na kuitwa wataalamu.

Leo hii tuna utitiri wa vyuo vikuu, lakini hatuna watu wenye ubunifu wa kidijitali na kiteknolojia, kwa sababu tuliwakaririsha kuchora miguu ya panzi na macho ya nzi, ambayo hayajatusaidia hata kuangalia twendako!

Tunakazania kufundisha watoto wetu kuwa zamani walikuwapo kina Kinjeketile Ngwale, Mkwawa, Mnyigumba na wengineo waliopambana na Wakoloni na kuwafurusha.

Wakati tukiwakaririsha hilo, hakuna hata mmoja anayeweza kutengeneza kompyuta au kishikwambi, ili mradi katika ulimwengu wa sasa maendeleo yako kwenye Sayansi na Teknolojia na si ile ya kupasua panya na vyura.

Ufike wakati sasa ikiwezekana kila shule iwe ya ufundi ambako watoto watafundishwa mambo ya kiufundi na teknolojia wakiwa wadogo ili hatimaye wakikua wawe wamezoea mambo hayo kuliko kufundishwa ukubwani.

Ndiyo sababu sasa tukianzisha miradi mikubwa tunajikuta tukiomba misaada ya wageni kutusaidia kuiendesha, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vyombo vya usafiri, tukishindwa kuvimudu hata kuomba kusaidiwa.

Tunashuhudia sasa maendeleo ya kiteknolojia yanakuja kwa kasi sana hata sasa kufikia hatua ya matumizi ya akili mnemba, ambayo inahitaji watu kupata elimu mpya ya jinsi ya kuisimamia na kuitumia katika masuala ya maendeleo.

Tuachane sasa na masuala ya Sayansi nyepesi nyepesi ya kufundishana sehemu za miili ya wadudu, ndege na wanyama na badala yake tujikite kwenye Sayansi na Teknolojia ya sasa ya kidijiti, ili twende na wenzetu wanaokimbia wakati tukitembea.

Jambo la msingi ni kujitahidi kukimbia nao kivitendo na kuachana na nadharia za makaratasi ya kutambua miaka ya darasani inayothibitishwa na vyeti badala ya ubunifu. Bila kufanya hivyo, Dunia itatuacha na kurudi kwenye Ujima. Mpo?

BIASHARA

# Wanawake Tabora walivyojitosa kwenye mapori kufuga nyuki

**Na Christina Mwakangale**

KINAMAMA mkoani Tabora, wamethibitisha kuwa wanawake wanaweza na kuvunja mwiko kuwa kazi za kuchonga na kutundika mizinga ya nyuki ni za wanaume.

Mwalimu mstaafu Joyce Nducha, anayeongoza kundi la wanawake zaidi ya 120, wafuga nyuki wenye mizinga zaidi ya 600, anaiambia Nipashe kuwa wameunda umoja unaoshirikisha kinamama kutoka wilaya zote tano za mkoa huo.

Anasema awali walikumbana na changamoto lakini sasa wamefanikiwa, wanamudu huduma muhimu za familia zao na kuongeza mapato binafsi.

Joyce anasema katika mazungumzo kuwa umoja huo una wanachama kutoka wilaya tano za mkoa huo ambazo ni Kaliua, Tabora Mjini, Uyui, Nzega na Sikonge. Anasema uongozi wa mkoa unawaunga mkono kwa kuwapatia mizinga 200 yenye thamani ya Shilingi milioni 16 kila mmoja ukiuzwa Sh. 80,000 na kwamba wameitundika kwenye pori la Ndewela na Igombe wilayani Uyui.

Anaeleza kuwa wameendelea na shughuli hiyo ila waliongeza kasi ya kuitundika kwa wingi baada ya kujiunga na kuunda kikundi mwaka jana.

Anaongeza kuwa wameanza kupata mavuno msimu huu mwaka (2024) kwa kuvuna madumu 30 yenye ujazo wa lita 20 kila moja na wameendelea kuchanga fedha zaidi kukuza mtaji kila mwanachama akitoa Sh. 20,000 ya kununua mizinga.

Kwa sasa imefikia mizinga 600 pamoja na ile waliyopewa na serikali mkoani humo, anaongeza Mwalimu Joyce.

Katika mauzo sokoni Joyce anasema dumu moja la lita 20 huuzwa kwa Sh. 200,000 kwa bei ya rejareja huku bei jumla huuzwa kuanzia Sh. 120,000.

Anaongeza: "Tukaona tujiunge pamoja kwa sababu umoja ni nguvu. Pia namna ya kupata mafunzo itakuwa rahisi kwetu, kuliko kuwa mtu mmoja mmoja ni ngumu kufikiwa na wadau mfano Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo -SIDO," anafafanua.

Anasema mafunzo ya namna ya kufuga nyuki waliyapata kutoka SIDO kwa kushirikiana na Ofisi ya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Ufugaji Nyuki, Tabora na sasa wanasonga mbele.

"Tulijifunza namna ya kuitundika mizinga, ila wanyamapori ni kikwazo. Wezi nao ndio shida zaidi," anasema Joyce.



Joyce Nducha kwenye biashara ya asali. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**CHANGAMOTO**

Mwalimu Joyce analalamikia wezi wa asali wanaowarudisha nyuma na kukwamisha malengo yao. Wanarina asali na kuacha mizinga ikiwa tupu ambayo ni hasara kwao.

"Tatizo mizinga tumeiweka chini wanakoweza kuifikia kwa urahisi, tumeamua kuipandisha juu zaidi ili wanyama na wezi wasiifikie kwa urahisi."

Anasema kwa vile ni kinamama hawawezi kufanya kazi hiyo kwa urahisi ila wanawatafuta kinababa wakwee juu na kuifunga eneo wasiloweza kufika wanyama na wezi.

Anafafanua kuwa kukabiliana na tatizo hilo SIDO imewafundisha kutengeneza mabanda na kuifungia mizinga ndani na kuacha nafasi ndogo ya nyuki kuingia na kutoka kwenda kutafuta chakula, ila mabanda hayo ni gharama zaidi.

"Yaani eneo lote linawekwa seng'enge halafu nyuki watatoka nje kupitia matundu ya seng'enge. Ni gharama pia uweke zege. Mzinga ukiwa na nyuki unauingiza kwenye banda wakishakomaa asali inajaa," anasema.

Changamoto nyingine anazoztaja Joyce ni kung'atwa na nyuki kutokana na vifaa vichache vya kurinia asali, mfano 'ovaroli' huuzwa kwa Sh. 120,000 na kwamba SIDO iliwapatia 10 , japo wako wengi.

**MAFANIKIO**

Wanashiriki maonesho ya Saba Saba mfano mwaka huu na kwamba kuwapo wanachama 10 wa kikundi chao ni faraja kwa kuzionesha, kujitangaza na kuuza wanachozalisha.

Wanafurahia mafanikio na kinamama wenzake kwa kuweza kumudu huduma za kuifuatilia na kupata asali lakini pia serikali kutambua na kuwaunga mkono na pia familia zao kuwa nao bega kwa bega.

"Rasmi tumeanza mwaka 2018 siku zinavyokwenda tunaimarika. Kama kinamama tunajitahidi kuweka uwiano kwenye majukumu ya kifamilia na biashara."

Anasema alikuwa mwalimu akajiunga na ujasiriamali badala ya kulala tu nyumbani na kuanzisha mradi huo.

Joyce anasema kwa umoja huo fursa nyingi zinawasogelea kwa mfano kupata mafunzo kwa pamoja, kuungwa mkono na serikali mfano ofisi ya mkuu wa mkoa.

# Haya ni machache usiyoyajua ndani ya treni ya umeme 'SGR'

**INATOKA UK.11**

**KUANDIKWA HISTORIA**

Ndoto ya muda mrefu ya Watanzania kuwa na usafiri wa treni ya kisasa ya umeme itakayoyaunganisha maeneo ya kimkakati kiuchumi na kusafirisha shehena za kitaifa na kimataifa ilionekana mwaka huu.

Ilianza rasmi Julai 14, mwaka huu ikitoka Dar es Salaam hadi Morogoro na ilipofika Julai 25, ilifika hadi Dodoma.

Rais Samia alipozindua usafiri huo, anasema uwapo wa usafiri wa kutumia reli hiyo utapunguza muda wa kusafiri kwa asilimia 60 kutoka wastani wa saa nane mpaka saa tatu, itapunguza ajali na msongamano wa magari kwenye barabara kubwa na pia kulinda mazingira kutokana na matumizi ya umeme badala ya nishati ya mafuta.

Anasema SGR itapunguza msongamano wa shehena kwenye bandari ya Dar es Salaam inayohudumia ushoroba wa kati (Central Corridor) hasa nchi za Rwanda, Burundi na DRC.

Kadhalika, anasema reli hiyo imeongeza kujiamini kwa Watanzania kwamba wanaweza kufanya miradi mikubwa yenye kuleta tija kwenye maendeleo ya taifa na kuwa na uchumi shindani.

Aidha, anasema serikali imeagiza mabehewa 1,430 ambayo yatabeba shehena ambayo itapitia kwenye ushoroba wa kati na kulitaka Shirika la Reli (TRC) kufungamanisha shughuli za reli na za maendeleo katika ushoroba huo.

**HISTORIA YA SGR**

Rais anasema: "Historia ya ujenzi wa SGR siyo tu inatoa tafsiri ya halisi ya kazi iendelee, inakumbusha maendeleo ya nchi ni hatua kwenye safari hiyo, kila awamu ya uongozi ina mchango wake."

Anafafanua kuwa mwaka 2001, Hayati Benjamin Mkapa, aliongoza kuandaa dira ya maendeleo ya miaka 25 iliyodhamiria kujenga Tanzania yenye uchumi imara na shindani ambapo ililenga kuwe na miundombinu itakayowezesha kufikia malengo kwenye sekta mbalimbali.

"Rais Mstaafu Jakaya Kikwete alifanya tathmini ya utekelezaji wa dira na kuamua itekelezwe kupitia mpango wa miaka mitano mitano, alitekeleza mpango wa kwanza.

Huu ulitoa kipaumbele cha ujenzi wa reli mpya na serikali ilifanya upembuzi yakinifu na tathmini ya kina ya ujenzi wa SGR na kukabidhi kwa mrithi wake,"anasema.

Aidha, anasema Hayati John Magufuli alianza utekelezaji wa mpango wa pili wa maendeleo ya taifa wa miaka mitano na ulibainisha reli kama mradi wa kielelezo na msingi wa mageuzi ya kiuchumi.

Anaongeza kuwa Mei 2017 serikali ilianza utekelezaji wa mradi huo kwa vipande viwili vya Dar es Salaam hadi Morogoro, na Morogoro hadi Makutupora Dodoma.

**TAZARA IMO**

Rais anabainisha kuwa serikali ipo katika hatua za mwisho za kufufua Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kuchangia shehena kwenye mradi wa SGR na kuweza kutumia bandari kavu kuunganisha miradi ya SGR na reli za waida (meter gauge railway - MGR).

Anasema ni muhimu kufungamanisha reli zote ikiwa ni pamoja na bandari kavu ya Kwala, Ihumwa na Isaka ili ziweze kuunganisha usafirishaji wa mizigo na shehena kutoka upande mmoja wa nchi mpaka upande mwingine.

Anaeleza kuwa, lazima kuwe na mifumo tofauti ya uendeshaji wa reli zote mbili yaani SGR na MGR ili kutambua ufanisi wa kila mfumo wa usafirishaji na kwamba hiyo italeta uwazi katika usimamizi wa mifumo hiyo ya reli.

Ameridhia stesheni ya Dodoma kuitwa Samia huku stesheni ya Dar es Salaam ikipewa jina la Dk. John Magufuli, kadhalika stesheni ya Morogoro itaitwa Jakaya Kikwete wakati ya Tabora itapewa jina la Ali Hassan Mwinyi.

Pia, stesheni ya Shinyanga imepewa jina la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Aman Karume, ya Mwanza itaitwa Julius Nyerere na Kigoma itakuwa Benjamin Mkapa.

**TRIL.10/- ZIMETUMIKA**

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa anasema zaidi ya Sh.Trilioni 10 zimetumika katika ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam-Morogoro-Dodoma chenye urefu wa kilometa 722.

Anasema kati ya fedha hizo trilioni sita sawa na asilimia 60 zimetolewa na Tanzania wakati trilioni nne sawa na asilimia 40 zimetolewa na wadau wengine wa maendeleo.

Waziri wa Uchukuzi anasema mbali na kukamilika kwa kipande hicho, serikali inaendelea na ujenzi wa vipande vingine vitano vya Makutupora-Tabora, Tabora-Kigoma, Mwanza-Isaka na Uvinza Msongati hadi kitega nchini Burundi na Kindu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).



# PPAA yaokoa bil. 567/- katika mashauri 140

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imesema imeokoa Sh. bilioni 567.6 katika mashauri 140 yaliyokuwa katika hatua mbalimbali za michakato ya ununuzi wa umma kwa kipindi cha miaka mitatu (2021 - 2024).

Katibu Mtendaji wa PPAA, James Sando amebainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari katika maonesho ya Kilimo ya Kimataifa (Nane Nane), yanayoendelea katika viwanja vya Nzuguni, Jijini Dodoma.

"PPAA imeendelea kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathmini ya zabuni.

Katika baadhi ya mashauri ambapo ilifanikiwa kubaini ukiukwaji wa taratibu za kufanya tathimini uliofanywa na taasisi nunuzi ikiwemo kutokuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kabrasha la zabuni au kuongeza vigezo vipya ambavyo havikuwepo awali," alisema Sando.

**"PPAA imeendelea kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathmini ya zabuni. Katika baadhi ya mashauri ambapo ilifanikiwa..."**

Sando alisema kwa kufanya hivyo mamlaka hiyo ilihakikisha kuwa zabuni zinatolewa kwa wenye sifa na hivyo kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha na kuepusha upotevu wa kiasi hicho.

Aidha, aliongeza kuwa PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa wazabuni 32 wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika na kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha.

Alisema mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Mamlaya ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imejenga moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kieletroniki.

Alisema moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko na kutoa fursa kwa wazabuni wengi kuwasilisha malalamiko yao.




Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania, Dk. Francis Alfred (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Thomas Bwana (kushoto), wakishiriki uzinduzi wa ulaji na unywaji wa bidhaa za korosho zinazozalishwa hapa nchini, uliofanyika kwenye banda la TARI, katika Maonesho ya Wakulima Nanenane, viwanja vya Nzunguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Uwekezaji miundombinu waleta neema wakulima, wafugaji, wavuvi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania, imesema uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya mawasiliano iliyofanya hususani katika maeneo ya vijijini umesaidia wakulima, wafugaji na wavuvi kupata taarifa rasmi za masoko ya bidhaa zao.

Meneja wa kampuni hiyo Kanda ya Kati, Salum Nguruas, alisema hayo jana alipokua akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya wakulima kitaifa yanayofanyika viwanja vya Nzuguni jijini hapa.

Ngururu alisema mawasiliano ni moja kati nyenzo muhimu katika kuwezesha wakulima, wafugaji pamoja na wavuvi kupata taarifa rasmi za mazao pamoja na masoko ya bidhaa zao.

"Kampuni yetu inatoa fursa na huduma mbalimbali za kilimo,ufugaji na uvuvi kama mtakumbuka Wizara ya Kilimo ilianzisha daftari la wakulima kwa ajili ya kupata ruzuku na njia inayotumika kuwapata ni mawasiliano kupitia namba zao za simu"alisema.

Alisema pia mawasiliano ya simu yanawasaidia wakulima, wafugaji pamoja na wavuvi kupata taarifa sahihi za aina gani ya mazao yanahitajika sokoni ili kuwafikia walaji.

Aidha, alisema ili kuwezesha makundi hayo yote kupata huduma za mawasiliano kampuni hiyo imekuja na utaratibu wa kukopesha simu janja kwa riba ndogo ambazo watazitumia kupata taarifa muhimu ikiwemo za ugani.

Kadhalika, alisema kupitia simu za mkononi wakulima, wafugaji na wavuvi wanaweza kukopa fedha kwa ajili ya kujipatia mitaji ya kuendesha shughuli zao bila kuwa na masharti ya dhamana yoyote.

# Miradi 10 ya bilioni 3/- yabainika na upungufu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imebaini upungufu kwenye miradi 10 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 3.1 katika maeneo mbalimbali.

Baadhi ya miradi iliyokutwa na upungufu ni pamoja na miradi ya elimu, afya pamoja na ujenzi wa barabaraba za ndani ya Jiji la Dodoma.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Eginius Hazinamwisho alisema hayo juzi kuwa katika uchunguzi wao walibaini nondo ambazo zilitumuka katika ujenzi wa madaraja na barabara hazikuwa na kiwango kilichotakiwa lakini mbao ambazo zilitumika hazikuwa na kiwango stahiki. Hazinamwisho alisema taasisi hiyo ilitoa taarifa katika sehemu husika na makandarasi kuamuliwa kuzitoa nondo hizo na kuleta zilizo na viwango bora vinavyotakiwa.

Alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi mbalimbali kutokana na taarifa zinazowasilishwa katika taasisi hiyo hapa nchini.

Hata hivyo, alisema moja ya vipaumbele vya taasisi hiyo kwa Mkoa wa Dodoma kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024 ni pamoja na kuelimisha umma kwa makundi tofauti ya wadau kuhusu madhara ya rushwa.

Alisema pamoja na utekelezaji wa majukumu yao ya kawaida pia wamejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele vinavyolenga kuzuia vitendo vya rushwa visitokee.

Katika hatua nyingine Hazinamwisho alitoa wito kwa kila mmoja kushiriki katika kuzuia vitendo vya rushwa. Hata hivyo, alisema kazi ya kupambana na rushwa ni ya kila mmoja hivyo jamii inapaswa kutoa taarifa kwa TAKUKURU ili waweze kukifanyia kazi suala la rushwa.

# Walengwa TASAF wawezeshwa kwenye Kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) umewawezesha wanufaika wanaojihusisha na kilimo, jambo lililochangia kuwaongezea kipato na kuzidi kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Kilimo ya Nanenane Mkoani Dodoma, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray alisema mfuko huo umekuwa ukitoa ruzuku kwa viwango tofauti kulingana na sifa ya mlengwa.

Alisema wapo ambao wameamua kuitumia katika kilimo na manufaa yameonekana, kwamba kuna walengwa kutoka Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma ambao wamelima mpunga, lakini wamehifadhi kusubiri bei ipande ili wauze kwa bei kubwa. "Wananchi tunaowahudumia wengi wao wanajihusisha na shughuli za kilimo, hivyo ruzuku tunazozitoa wanazitumia kwa makini kwa kugawa, kiasi wanatumia kwenye kilimo kwa kununua pembejeo na wengine wanatumia kwenye matumizi mengine, ki ukweli TASAF imesaidia sekta ya kilimo kwa asilimia kubwa," alisema Mziray.

Akitoa mfano, Mziray alisema: "Kwa mfano kule mkoani Njombe kupitia Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka amefanya ubunifu kwa kushirikiana na Mpango wa Kukuza Kilimo Kanda ya Kusini (SAGCOT), wameweza kuwapatia walengwa wa TASAF miche 10 bora ya parachichi kwa kila mmoja, tuliwatembelea baadhi yao na walengwa wameambiwa baada ya miaka mitatu watakuwa wametoka kwenye umaskini".

Aidha, alisema TASAF inaangalia namna ya kuungana na taasisi zingine zilizopo kwenye halmashauri, pamoja na Shirika la Viwanda Vidogo vidogo (SIDO) ili kuhakikisha bidhaa za walengwa zinakuwa na ubora na kuingia katika soko la ushindani.

Alisema pia wanahakikisha walengwa wanatengeneza bidhaa ambazo zimefanyiwa utafiti ili kuhakikisha zinapata soko bila shida.

Mwenyekiti wa taasisi ya Lisitu Agri Bussines iliyopo chini ya mwamvuli wa SAGCOT, Beno Mgaya, alisema wanachokifanya ni kuwaondoa walengwa katika mtazamo hasi wa kuonekana maskini wakati wanamiliki ardhi ya kilimo.

Mgaya alisema kwa kushirikiana na TASAF wamefikia zaidi ya walengwa 4,000 kutoka katika mikoa Dodoma, Mbeya, Morogoro, Njombe, Ruvuma, Rukwa na Kigoma.

Mmoja wa wanufaika wa mfuko huo kutoka Kijiji cha Mapilinga wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Mlengwa Magesa, alisema TASAF imekuwa neema kwao kwani ameweza kusomesha watoto wake wanne.





# Waliojenga milimani waikwamisha serikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wananchi jijini Mbeya wanaoishi kwenye maeneo yenye miinuko mikali wanaikwamisha serikali kufikisha baadhi ya huduma muhimu ikiwemo maji na umeme.

Kutokana na hali hiyo Halmashauri ya Jiji hilo imeshauriwa kuanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi utakaosaidia kulinda baadhi ya maeneo muhimu ikiwemo vyanzo vya maji na maeneo ya kilimo.

Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson alitoa ushauri huo juzi alipotembelea Mradi wa Maji wa chanzo cha maji Itagano unaotekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-UWSA) kwa zaidi ya Sh. bilioni 5.2.

Dk. Tulia alisema karibu na chanzo hicho kuna baadhi ya wananchi wanalima mazao mbalimbali kwenye maeneo yenye miinuko na wengine wameanzisha makazi hali ambayo inahatarisha uwepo wa chanzo hicho na tija ndogo ya kilimo.

Alisema wananchi waliojenga nyumba kwenye maeneo hayo yenye miinuko mikali wanapohitaji huduma ya maji na huduma zingine inakuwa gharama.

"Hatuwezi kuwazuia watu kulima ila tuwashauri wasilime mazao ya muda mfupi, tuwashauri wapande miti ambayo itasaidia kutunza vyanzo vyetu vya maji lakini tusiwaruhusu kujenga makazi," alisema Dk. Tulia.

**"Hatuwezi kuwazuia watu kulima ila tuwashauri wasilime mazao ya muda mfupi, tuwashauri wapande miti ambayo itasaidia kutunza vyanzo vyetu vya maji lakini tusiwaruhusu kujenga ..**

Alisema wakulima wanaolima kwenye miinuko mikali hata tija yake inakuwa ndogo kutokana na mbolea wanayotumia kusombwa na maji pamoja na kusababisha mmomonyoko wa ardhi.

Alisema yuko tayari kuwasambazia wananchi hao miti bila malipo yoyote ili waipande kwenye maeneo hayo badala ya kuendelea kupanda mazao ya muda mfupi.

Hata hivyo alipongeza mamlaka hiyo kwa kuboresha huduma kwa wananchi ikiwemo kufikisha maji kwenye maeneo ambayo wananchi walikuwa hawayapati pamoja na kubuni vyanzo vipya vya maji.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi wa Mbeya-UWSA, Gilbert Kayange alisema mradi huo unatarajiwa kuhudumia zaidi ya watu 40,000 wa Kata za Ilemi, Iganzo na Mwansekwa na kwamba mpaka sasa umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90.Alisema wananchi wameshaanza kunufaika na maji ya chanzo hicho kwa kuweka mfumo maalumu ambao unasaidia kupeleka huduma kwa wananchi wakati ujenzi ukiendelea.

Alisema mbali na chanzo hicho pia serikali inaendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira ambao unatarajiwa kumaliza tatizo la maji katika Jiji hilo, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na baadhi ya miji iliyo jirani na jiji hilo.

Alisema kwa sasa kiwango cha uzalishaji wa maji na kwamba kwa sasa upatikanaji wa maji umefikia zaidi ya asilimia 90 na wanaendelea kubuni vyanzo vipya.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu kiwango cha uzalishaji wa maji kimeongezeka kutoka lita za ujazo milioni 38 mpaka lita milioni 68 na kwamba ongezeko hilo limetokana na serikali kuwekeza fedha nyingi kwenye ujenzi wa miradi ya maji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mbeya-UWSA, Edna Mwaigomole aliishukuru serikali kwa kuidhinisha fedha kwa ajili a utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.



Daktari Salim Mohammed kutoka Hospitali ya Medwell ya Kibaha, mkoani Pwani, akimfanyia vipimo vya macho Charles Aloys, aliyejitokeza kwenye kambi ya siku tatu ya upimaji wa afya na macho, iliyoandaliwa na Jumuiya ya Shia Khoja Ithnaashari katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda cha Ifodi kuzalisha mipira ya kiume

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KIWANDA cha kutengeneza mipira ya kuvaa mikononi (glavu) cha Bohari ya Dawa (MSD) kilichopo eneo la Idofi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe kinatarajiwa kuanza uzalishaji wa mipira ya kiume (condom).

Hayo yalieelezwa juzi na Meneja Mipango Tathmini na Ufuatiliaji, Hassan Ally kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa MSD mbele ya Kamati ya Kudumu Bunge ya Afya na Ukimwi ilipofanya ziara kiwandani hapo.

Alisema uzalishaji wa mipira ya kiume utaokoa fedha za serikali takribani Sh. bilioni 50 ambazo zinatumika kununuwa bidhaa hiyo nje ya nchi.

Alibainisha kwamba, fedha inayotumika kununua mipira ya kiume nje ya nchi ni nyingi na wakati mwingine zimekuwa zikiletwa kwa msaada, kwamba wanaotoa msaada wenyewe wameanza kuhimiza viwanda kujengwa kwenye nchi zinazopokea ili zianze kuzalisha bidhaa hiyo.

Hata hivyo, alisema kwa sasa kiwanda cha MSD Idofi kimeanza uzalishaji wa mipira ya mikono ambapo kwa kipindi cha miezi mitano tangu Februari mwaka huu mipira milioni nne yenye thamani ya Sh. bilioni 1.14 imezalishwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Ukimwi, Christina Mzava aliwataka MSD kuhakikisha uzalishaji wa kiwanda hicho unafikia asilimia 100 kwa kuwa sasa kiwanda kinazalisha mipira ya mikono, huku ikisalia mipira ya mikono ya upasuaji.

wajumbe wa kamati hiyo akiwemo, Seif Salim Seif ambaye ni mbunge wa Mtambile Pemba alipongeza uwekezaji huo, lakini pia alishauri kuongezwa kwa teknolojia za mitambo ya automatiki katika idara zote pamoja na kuzingatia afya za wafanyakazi ikiwemo kuongeza wigo wa hewa safi ndani ya kiwanda hicho.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alisema zinahitajika zaidi ya shilingi bilioni mbili ili kuongeza aina ya pili ya mipira hiyo ya mikono.

Ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mipira ya mikono cha Idofi kimetumia Sh. bilioni 12.4 na sasa kimeanza uzalishaji na kupeleka bidhaa sokoni za Sh. bilioni 1.2.

# Waomba bima ya afya kwa wote kuanza haraka

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

WANANCHI mkoani Njombe wamesema ni muhimu zoezi la upatikanaji wa bima za afya kwa wote likafanyika haraka, kwamba imekuwa na faida kubwa kutokana na hali ya uchumi wa sasa.

Aidha, alisema wamekuwa wakipata adha pindi wanapokuwa wagonjwa huku wakiwa hawana fedha na kujikuta wanageuka kuwa omba omba kwa ndugu.

Walitoa ushauri huo juzi baada ya ziara ya Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware na baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo katika Mkoa wa Njombe ikiwa ni mwendelezo wa ziara katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Baadhi ya wananchi hao akiwemo, Ignas Lyimo alisema kuwa bima ya afya ni muhimu kwani hawawezi kuwa na fedha wakati wote hivyo wakiwa nayo itawasaidia.

"Mimi kama fundi sina hela muda wote ya kukidhi gharama za matibabu kwa hiyo ninaona ni muhimu kuwa na bima ili kipindi ambacho nitakuwa na matatizo ya kiafya inisaidie," alisema Lyimo.

Hynes Mbaji alisema kuwepo na bima ya afya ni muhimu kwa sababu inaweza kusaidia wakati ambao hauna fedha za kwenda hospitali kupata huduma.

Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware alisema mchakato wa kuanza kwa bima ya afya kwa wote unaendelea na kinachosubiriwa ni kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Bima Sura Namba 394 Kifungu Kidogo cha 5.

"Mwananchi anaweza akanunua bima ya afya NHIF, anaweza akanunua CHF, pia anaweza akanunua kampuni binafsi ambazo zinatoa bima ya afya na akishakuwa na kadi huyo tayari anahesabika ametii sheria," alisema Saqware.

Naye Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Edward Mwakipesile alisema wapo tayari kuhamasisha wananchi na kuwapa elimu ya umuhimu wa bima ya afya, hivyo mamlaka hiyo ijitahidi kuharakisha mchakato wa kanuni.

Alisema pia walianza kutoa elimu katika Kijiji cha Mundindi wilayani Ludewa chenye wakazi 3149, ambao walipewa fidia na serikali kupisha mradi wa Liganga na Mchuchuma ambao tayari wote wamekatiwa bima za afya.



# Kauli za chuki, ubaguzi zamkera Dk. Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema haridhishwi na kauli za chuki na ubaguzi zinazotolewa na viongozi wa vyama vya upinzani.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa kamati za siasa za ngazi ya matawi hadi mkoa katika Mkoa wa Mjini na kusema kuwa kauli hizo za wapinzani zinaashiria uvunjifu wa amani katika nchi.

Alisema nchi imetulia kutokana na kuwa na amani lakini hivi karibuni kumeanza kuibuka tabia ya baadhi ya vyama vya siasa kutumia vibaya majukwaa ya mikutano ya hadhara kwa kutoa kauli zinazoashiria chuki na ubaguzi.

Hivyo aliwataka wanachama wa CCM kuendelea kuhubiri amani.

Dk Mwinyi alisema wapo baadhi ya viongozi watatoa kauli za uongo na upotoshaji kuhusu miradi mbalimbali inayotekelezwa nchini ikiwemo Bandari na Uwanja wa Ndege Pemba na kusema kuwa miradi hiyo imeuzwa na kuzua taharuki kwa wananchi jambo ambalo siyo kweli.

Aidha alisema serikali ilifanya uchunguzi wa kina na kuona umuhimu wa maeneo hayo kuwapa wawekezaji na kwamba kutasaidia kuongeza pato la taifa. Alisema kwa sasa mamlaka ya uwanja wa ndege inakusanya shilingi bilioni 40 kwa mwaka wakati hapo awali ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 12 pamoja na kutoa huduma bora, hali iliyopelekea kutangazwa kuwa kiwanja bora Afrika.

**Akizungumzia kuhusu Bandari, Dk. Mwinyi alisema awali makusanyo yanayotokana na bandari yalikuwa shilingi bilioni 36 lakini kwa sasa yameongezeka hadi shilingi bilioni 51 .**

Akizungumzia kuhusu Bandari, Dk. Mwinyi alisema awali makusanyo yanayotokana na bandari yalikuwa shilingi bilioni 36 lakini kwa sasa yameongezeka hadi shilingi bilioni 51 ndani ya miezi tisa pekee.

Hata hivyo alisema serikali kupitia utekelezaji wa ilani ya CCM imevuka lengo la utekelezaji wa ilani hiyo kutokana na kutekeleza miradi mingi ikiwemo sekta ya afya, elimu pamoja na miundombinu ikiwemo ujenzi wa masoko ya kisasa. Katika hatua nyingine Dk. Mwinyi aliwataka viongozi wa CCM kuanzia ngazi za matawi kujipanga kwa kuhakikisha wanajiandikisha katika daftari la wapiga kura, akisema chama kipo tayari kutoa msaada ili kufanikisha uandikishaji daftari kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Akitoa taarifa ya utekelezaji wa CCM, Katibu wa CCM Mkoa wa Mjini, Innocent Nanzaba, alisema mkoa tayari umesajili wanachama zaidi ya milioni moja katika mfumo wa kieletroniki.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini, Talib Ali Talib alisema maendeleo makubwa yamepatikana kutokana na miradi mingi ya kimkakati ipo katika mkoa huo.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa wakulima wa mboga na matunda, alipotembelea Maonesho ya Wakulima ya Nane Nane, katika viwanja vya Dole, Zanzibar jana. **PICHA: OMPR**

## Vijana watakiwa kuilinda, kuitunza miundombinu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Abdi Mahmoud, amewataka vijana kuilinda na kuitunza miundombinu ya Barabara.

Alisema hayo jana baada ya kumaliza matembezi ya vijana visiwani Zanzibar, kueleza kuwa Rais Dk. Mwinyi anafanya jitihada kubwa katika kuiletea maendeleo nchi kwenye nyanja zote ikiwa pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji nchini.

Alisema Serikali ya Zanzibar imedhamiria kufanya mageuzi makubwa katika uimarishaji wa miundombinu Unguja na Pemba ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, ambapo ujenzi wa miundombinu hiyo ina lengo la kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi.

Alisema vijana wapo tayari katika kulitumikia taifa na wamejiandaa kushinda katika uchaguzi mkuu wa mwakani na wapo imara katika kulilinda taifa.

"Barabara hizi zimejengwa kwa gharama kubwa tunawaomba watumiaji wa barabara wakiwemo vijana kuhakikisha wanafuata sheria za barabarani na kuzilinda na kuzitunza barabara ili zitumike kwa muda mrefu nan chi kuendelea kupata maendeleo" alisema.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulghulam Hussein alisema vijana wanakila sababu ya kujivunia maendeleo yanavyofanywa na Rais Dk. Mwinyi na kuwataka kuendelea kumuunga mkono ili kuendelea kuleta maendeleo nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Mji Magharib Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa aliwataka vijana kujitokeza kwa wingi ktika viwanja vya Amani kumuunga mkono Rais Dk. Mwinyi katika tamasha la vijana wa UVCCM litakalofanyika Agosti 10 mwaka huu.

Alisema CCM inahadhina kubwa ya vijana imara hivyo ni vyema kuendelea kuhubiri na kudumisha amani na usalama wa nchi lakini pia kuungana kwa pamoja katika kuhakikisha wanakipatia ushindi chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

# Serikali yatoa ufafanuzi tuhuma ujenzi wa miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetoa ufafanuzi kuhusu tuhuma zilizotolewa na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu kuhusu ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa Barabara ya Chake-chake-Wete Pemba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhamed alisema, tuhuma zinazotolewa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa hazina msingi na ukweli wowote.

Alisema hata wananchi wanaoishi na kutumia barabara hiyo wanaziona changamoto za mkandarasi huyo.

Waziri huyo alisema madai yaliyotolewa na kiongozi huyo ya kwamba, mkandarasi huyo alikataliwa asipewe kazi kwa sababu kuna watu walitaka wapewe fedha ni ya upotoshaji, uzushi na yenye nia ya kuchafua na kuwagombanisha wananchi na serikali yao.

"Ni vyema ieleweke kwamba, serikali ndio iliyosaini mkataba na mkandarasi huyu bila ya kulazimishwa na mtu yeyote.Tuhuma nyingine iliyotolewa ni kucheleweshwa malipo kwa mkandarasi, tunaomba ifahamike kwamba, taratibu za malipo kimkataba kwa mkandarasi huanza kwa kulipwa malipo ya awali na malipo hayo yalifanyika kikamilifu kwa mujibu wa mkataba"alisema Dk. khalid.

Alisema madhumuni yake ni kumwezesha mkandarasi kuanza maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi ikiwemo uletaji wa vifaa na wataalamu, jambo ambalo hadi muda wa utekelezaji wa mradi huo unamalizika, mkandarasi ameshindwa kukamilisha utekelezaji wa kipengele hicho.

Aidha alisema pamoja na kutokutekeleza kipengele hicho, mkandarasi bado aliendelea kulipwa malipo ya pili, ya tatu yalichelewa kulipwa kwa siku 160 baada ya Benki ya M Maendeleo ya Kiarabu (BADEA) na Mfuko wa Saudi Fund kutoridhishwa na maendeleo ya ujenzi huo.

Alisema kwamba ucheleweshaji huo haukutokana na Serikali bali ulitokana na mlipaji kutoridhishwa na utendaji wa mkandarasi na malipo ya tatu yalifanyika baada ya ujumbe kutoka Saud Fund na BADEA kuja Zanzibar Desemba mwaka 2023 na kutembelea eneo la mradi pamoja na kufanya mkutano na menejimenti ya Wizara na hatimaye kufikia makubaliano ya kimaandishi ya kurekebisha kasoro zilizobainika.

Waziri huyo alisema moja ya mambo yaliyotakiwa na Saud Fund na BADEA kwa mkandarasi huyo ni kuufanyia mapitio mpango wake kazi ili uendane na uhalisia wa utekelezaji wa mradi, jambo ambalo hadi sasa hajaweza kulikamilisha.

Kuhusu malipo ya fidia kwa vipando na nyumba za wananchi, Dk Khalid alisema hilo nalo siyo tatizo kwani asilimia 95 ya wananchi wote wanaostahiki kulipwa fidia wameshalipwa malipo yao kwa mujibu wa sheria na taratibu za malipo ya fidia.

Alisema eneo la mradi ambalo limeshalipwa fidia, ni eneo la kutosha kwa mkandarasi kulifanyia kazi kwa zaidi ya asilimia 90, hivyo tuhuma inayotolewa na baadhi ya viongozi wa kisiasa ya wananchi kutokulipwa malipo ya fidia zao siyo sahihi na za upotoshaji.

Akizungumza Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, alisema kiwanja hicho kinajengwa kwa kiwango na hadhi ya kimataifa ili kuifungua Pemba kiuchumi ambayo ndio dhamira ya dhati ya Rais Dk. Mwinyi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

Alisema Serikali imechukua juhudi kubwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kupata mkopo wa Euro Milioni 170 kutoka United Kingdom Export Finance (UKEF) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Hata hivyo alisema hapo awali, mjenzi wa mradi huo ilikuwa ni ubia wa Kampuni ya PROPAV ya nchini Brazil na MECCO na fedha za malipo ya awali zimeshalipwa kupitia Benki ya CRDB ambapo wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi kulijitokeza kutofahamiana kwa wabia hao wawili na kusababisha mgogoro pamoja na kufikishana mahakamani.

Alisema jambo hilo lilipelekea mahakama kutoa amri ya kusitisha utekelezaji wa mradi hadi hapo shauri lao litakaposikilizwa na kuamuliwa.

# Wawili zaidi mbaroni madai ya kuzusha kifo binti aliyebakwa

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Mkoani Arusha linawashikilia watu wawili, kwa tuhuma za kusambaza taarifa za uongo katika mitandao ya kijamii za kumzushia kifo binti aliyefanyiwa ukatili kwa kulawitiwa na kubakwa.

Agosti 4, mwaka huu, katika mitandao ya kijamii kulisambaa video ikionesha vijana watano wanaodaiwa kuwa askari, wakimfanyia ukatili huo binti huyo mkazi wa Yombo Dovya, Temeke mkoani Dar es Salaam huku wakimrekodi.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, SACP Justine Masejo, ilisema jeshi hilo linawashikilia Venance Malya (54), mkazi wa Sombetini na Izack Elias (44), mkazi wa Daraja Mbili, jijini humo kwa tuhuma za kusambaza taarifa hizo za uongo katika mitandao ya kijamii kuwa binti huyo amefariki dunia suala ambalo si kweli.

Kamanda Masejo lisema wanaendelea na upelelezi wa shauri hilo na utakapokamilika jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

"Tunatoa wito kwa watu kujiepusha kutoa, kusambaza ama kuchapisha taarifa za uongo katika mitandao ya kijamii kwa lengo la kuleta taharuki, hofu au kutafuta umaarufu katika jamii," alisema.

Kamanda Masejo alisema kufanya hivyo watambue kuwa ni makosa na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Watuhumiwa hao wanafikisha idadi ya watu watatu waliokamatwa kwa madai hayo baada ya kuzi Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, kumkamata Amos Lwiza (54).

**MWANASAIKOLOJIA**

Mwanasaikolojia-Tiba, Saldin Kimangale, alisema asilimia 20 hadi 30 wanaopitia madhila ya ukatili kama wa binti huyo hupata changamoto katika afya yao ya akili kwa kupata msongo, ukiwewe au hofu baada ya janga.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Kimangale alisema mtu yeyote anayepata janga linaweza kuwa la ukatili, ajali, tetemeko au mafuriko kushindwa kurudi katika hali yake ya kawaida na kuwa na wasiwasi na sononа.

"Watu wanaopitia hali hizi aghalabu baada ya muda hureja katika hali zao za kawaida hasa wakipata msaada wa kihisia kutoka kwa watu wa karibu.

"Hata hivyo asilimia 20 hadi 30 huwa wanapata changamoto katika afya yao ya akili kwa kupata msongo, ukiwewe au hofu baada ya janga na kushindwa kurudi katika hali ya kawaida kutokana na wasiwasi na sonona," alisema.

Alisema wako pia katika hatari ya kusitisha uhai kwa sababu ya kutawaliwa na hisia za kutokuwa na thamani, aibu na hatia. Msaikolojia huyo alishauri kuwa ni vyema kupatiwa huduma ya afya ya akili mapema ili kuzuia changamoto hizo zisijitokeze.

"Utafiti mbalimbali unaonesha kuwa hata baada ya mwaka mmoja kupita mwathirika anaweza kupata ukiwewe (PTSD) kwa sababu ya vichocheo vya kimazingira na uwapo wa kumbukumbu na kwa sababu pia, maumivu ya kihisia hujikusanya kila panapopatikana kumbukizi," alisema.

Alisema binti huyo na waathirika wengine wanapaswa kupatiwa huduma za afua mapema kabla hajapata ugonjwa kamili wa akili.



Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA bara, Tundu Lissu. **PICHA: MTANDAO**

# Tundu Lissu atishia kuikacha CHADEMA ikizingua

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema iwapo chama hicho kitaacha misingi iliyomfanya kujiunga nacho kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, anaweza kuondoka.

Lissu aliyesema hayo katika mjadala mtandaoni jana, baada ya kuulizwa na mmoja ya wachangiaji iwapo angeendelea ~~kubaki ndani ya chama hicho~~ katika mazingira yoyote ikiwemo kutofautiana kwa kiasi kikubwa na viongozi wenzake.

"Mwalimu (Julius) Nyerere kati ya mojawapo ya kauli zake nyingi aliwahi kusema CCM siyo mama yangu na ikiacha misingi yake nitaiacha. Hiyo ilikuwa kauli ya Mwalimu kuhusu chama alichokianzisha.

"Wewe unataka mimi niseme kwa mazingira yoyote yale, vyovyote itakavyokuwa sitahama. CHADEMA je ni mama yangu?" alihoji Lissu na kujibiwa kuwa chama hicho si mama yake.

"Sasa kama siyo mama yangu niliingia CHADEMA miaka 20 iliyopita na Mungu anisaidie niendelee kuwa CHADEMA kwa kadri itakavyowezekana lakini CHADEMA siyo dini na siyo mama yangu ni chama cha siasa. Ikiacha misingi yake iliyonipeleka nikajiunga nacho nitaondoka nitakuwa sina sababu ya kubaki," alisema Lissu.

Hivi karibuni alitangaza nia ya kuwania urais kupitia chama hicho endapo angepewa ridhaa jambo ambalo liliibua mjadala ndani na nje ya chama hicho kwa wale wanaomuunga mkono katika azma yake hiyo na wale wanaompinga na kumpa nafasi Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe.

Mbowe na Lissu wote wamewahi kugombea nafasi hiyo kwa nyakati tofauti. Mbowe aligombea mwaka 2005 na kushika nafasi ya tatu nyuma ya Rais mstaafu Jakaya Kikwete na Ibrahim Lipumba kutoka Chama cha Wananchi (CUF).

Lissu aliwania urais kwa mara ya kwanza mwaka 2020 dhidi ya Hayati Dk. John Magufuli wa CCM katika uchaguzi ambao ulilalamikiwa na upinzani ikiwamo CHADEMA na wadau wengine kwamba haukuwa huru na haki huku mgombea wa CCM akitangazwa mshindi na Lissu kushika nafasi ya pili.

## Kisarawe yapunguza vibali uvunaji misitu

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani imepunguza kutoa vibali vya uvunaji misitu kutoka 198 kwa mwaka 2023 hadi 95 vya mwaka huu, ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Makusanyo yake ya mapato ya mazao ya misitu yamepungua kutoka Sh. milioni 800 hadi 350 kwa mwaka kutokana na namna walivyokuwa wakitoa vibali vya uvunaji.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa Misitu Msaidizi wa Halmashauri hiyo, Waziri Mkumbwa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hali halisi ya udhibiti wa ukataji miti kwenye misitu ya wilayani humo.

"Hali ya uvunaji misitu imekuwa ikiongezeka mara kwa mara kutokana na uvunaji wa mazao ya misitu kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa, hali hii imesababisha kujipanga kudhibiti uvunaji kwa kutoa vibali vichache," alisema.

Alisema kiwango hicho cha uharibifu wa misitu kitashuka zaidi kwa kuwa hivi sasa wanashirikiana na wadau mbalimbali, zikiwamo Taasisi ya TaTEDO-SESO ambayo inatekeleza mradi jumuishi wa kuhifadhi misitu na kuboresha mnyororo wa thamani wa mkaa.

Mratibu wa mradi huo, Shima Sago alisema mradi huo wa miaka mitatu unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kusimamiwa na Wizara ya Fedha, ukilenga kujengea jamii uwezo wa kutunza na kusimamia misitu na mnyororo wa mkaa kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi.

"Tumewafindisha wanapochoma mkaa wazingatie kuwa na matanuru ambayo kuna sehemu maalumu ya kutolea moshi usio na athari kwa afya zao, lakini pia tanuru bora ambalo linatoa mkaa mwingi tofauti na awali," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

# Ubalozi wa Tanzania Uingereza wataka ulinzi Mtanzania anayetishiwa maisha

**Maulid Mmbaga na Moshi Lusonzo**

BALOZI wa Tanzania nchini Uingereza, Mbelwa Kairuki, ameitaka Uingereza kumhakikisha usalama Martina Farrall mwenye asili ya Tanzania.

Martina Farral,amelalamika kutishiwa kuuawa, kuteswa na kunyang'anywa watoto na mume wake, ambaye jina halikutajwa raia wa nchi hiyo.

Wiki hii kulisambaa mitandaoni video fupi ikimuonesha Martina, akiomba msaada kutokana na mume wake ambaye anaishi naye eneo la Ireland ya Kaskazini, kumpa vitisho vya kumuua, kumnyang'anya watoto na kumtesa.

Katika taarifa ya Balozi wa Tanzania nchini Uingereza, Mbelwa Kairuki, alisema baada ya kuiona video hiyo tayari wamechukua ikiwamo kuitaka serikali ya nchi hiyo kumhakikishia usalama wake pamoja na kutuma timu ya maofisa wake kwenda kumtafuta eneo alilokuwepo.

Balozi Kairuki alisema ofisi yake amewasilisha taarifa ya Martina kwa Mamlaka za Uingereza na kuomba hatua za kufuatilia suala hilo zichukuliwe mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha usalama wake sambamba na kufanyia kazi shutuma alizotoa ili kubaini ukweli wa shutuma hizo na hatua kuchukuliwa.

"Aidha, leo (Agosti 6), Ofisa Ubalozi wa Tanzania anakwenda Ireland ya Kaskazini katika Mji anapoishi Farrall ili kukutana na Mamlaka zinazohusika kufuatilia suala hilo" alisema Balozi Kairuki.

Katika video iliyorekidiwa, alionekana Farrall, akiomba Watanzania na serikali ya Uingereza kufahamu anachopitia baada ya mume wake kumpatia mateso mengi ikiwamo kumpeleka katika hospitali ya magonjwa ya akili, kumuondoa ndani ya nyuma, kumtenganisha na watoto wake wanne na kumtishia kumuua.

"Watanzania wezangu nashukuru na simu zenu, nataka niwaeleze jambo mume wangu amewachukua watoto wangu na kunitishia ataniua kama nisipoondoka," alisema Farrall kupitia video hiyo.

Alisema mume wake kwa kushirikiana na polisi wa eneo hilo walisuka mpango wa kumkamata na kumweka mahabusu na walipomwachilia walimtaka aondoke nchini humo kwa kuwa yeye sio raia wa Uingereza.

Alisema watoto wake wanne wawili wanaume na wengine wanawake, mume wake amewachukua na haruhusiwi kuwaona kwa kuwa yeye ni mweusi.

Farrall alieleza kuwa aliamua kurekodi video hiyo ili kuwajulisha Watanzania kuwa yuko kwenye na matatizo na hata akipoteza maisha atakuwa ameweka wazi jambo hilo.

Aidha, Watanzania wanaoishi nchini Uingereza wamesisitizwa kuchukua tahadhari kutokana na sintofahamu iliyozuka ikisababishwa na baadhi ya watu waliotoa hoja ya kutaka wageni kuondolewa katika taifa hilo.

Machafuko yalizuka nchini Uingereza siku chache zilizopita baada ya kuonekana kwa mkanda wa video uliomwonesha mtu mmoja aliyeripotiwa kuwa mwomba hifadhi akiwachoma kisu wasichana wadogo kwenye mji wa Southport Julai 29, mwaka huu.

"Ubalozi utakuwa tayari kuwasaidia watanzania endapo kutatokea hali ya dharura mpaka pale hali itakaporejea kawaida. Mtu mwenye uhitaji awasiliane na ubalozi kwa kutuma barua pepe kupitia UBALOZI@TZHC.UK" UBALOZI@TZHC.UK au simu +44 20 7569 1470, +44 7880 870 540, na +44 7909 323 286," ilisema sehemu ya taarifa ya Ubalozi.

Ilielezwa kuwa, mamia ya waandamanaji kwenye miji kadhaa nchini humo walipambana na polisi, huku wakivunja madirisha ya hoteli ambazo zimewapatia makazi waomba hifadhi kutoka Afrika na Mashariki ya Kati, huku wakiwataka kuwaondoa na kuzuia boti za wahamiaji zinazowasili nchini humo.

Waziri Mkuu wa Uingereza Kier Starmer, aliwaonya waandamanaji kuwa huenda wakakabiliwa na vifungo vya muda mrefu jela, wakati akijaribu kuondoa ghasia mbaya zaidi kuwahi kutokea nchini humo ndani ya miaka 13. Akisisitiza kwamba jukumu lao kuu ni kuhakikisha jamii ziko salama.

Pia, wa mujibu wa vyombo vya habari nchini humo, maelfu ya watu wanaopinga ubaguzi huo wa rangi, waliandamana jana kwenye miji mbalimbali kulaani uvamizi na fujo dhidi ya wageni uliotekelezwa siku chache zilizopita na watu wanaodaiwa kuchochewa na wanasiasa wenye mrengo wa kulia.

Maandamano hayo yalifanyika katika jiji kuu la London na miji mingine kama Bristol na Newcastle ambapo, waandamanaji walibeba mabango na kusema wahamiaji na waomba hifadhi wanakaribishwa nchini Uingereza.

## Iran yasisitiza itajibu mauaji ya Haniyeh

**JEDDAH,** Saudi Arabia

WAKATI wanadiplomasia wa mataifa mbalimbali wakitafuta namna ya kuepusha vita Mashariki ya Kati, Iran imesema nia yake ya kulipiza kisasi kwa Israel itabaki palepale.

Kaimu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Baqeri Ali Bagheri Kani, alisema nchi yake itajibu mauaji ya kiongozi wa Hamas Ismail Haniyeh katika wakati na njia inayofaa.

Kani alitoa kauli hiyo wakati wa mkutano wa dharura wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC), uliofanyika nchini Saudi Arabia kujadili jibu nchi ya Iran la kulipiza kisasi kwa Israel kutokana na mauaji hayo.

Hata hivyo, Marekani ilisema ina matumaini na nchi wanachama wa OIC, kuwa wataionya Iran kuhusu kuchukua hatua hiyo na kuzidisha mzozo huo. Mvutano katika Mashariki ya Kati umeongezeka tangu kuuawa kwa Haniyeh katika mji wa Tehran nchini Iran wiki iliyopita. Israel ililaumiwa kuhusika na mauaji hayo, lakini haijazungumza chochote.

Mkutano huo wa OIC ilifanyika Jumatano katika mji wa Jeddah.

Kaimu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, aliwaambia wanachama wa jumuiya hiyo kuwa nchi yake inatarajia kwamba wanaunga mkono jibu la Iran kwa mauaji hayo.**BBC**



Kiongozi mpya wa Serikali ya mpito wa Bagladesh, Muhammad Yunus, akiwasili nchini humo siku chache baada ya Waziri Mkuu Sheikh Hasina kukimbia nchi. **PICHA: REUTERS**

## Biden aonesha hofu Trump kukubali matokeo

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema hana imani kuwa kutakuwa na hali ya amani iwapo kiongozi wa zamani wa nchi hiyo, Donald Trump atashindwa katika uchaguzi wa urais unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu.

Katika mahojiano yake ya kwanza tangu alipojiondoa katika kinyang'anyiro hicho mwezi uliopita, Rais Biden alikiambia kituo cha CBS News kuwa, ikiwa Trump atashindwa, hana imani hata kidogo kama atakubaliana na maamuzi ya sanduku la kura.

"Trump anamaanisha anachosema, hatumchukulii kwa uzito.Anamaanisha hivyo, mambo haya yote kuhusu kauli yake kuwa akishindwa kutakuwa na umwagaji damu." Alisema.

Kauli ya Trump kwamba kutakuwa na umwagaji damu nchini humo ikiwa atashindwa katika uchaguzi, yaliyotolewa alipokuwa akizungumza na wadau wa sekta ya magari mwezi Machi, na kusababisha ukosoaji kutoka kwa watu mbalimbali.

Wanachama wa Democratic walikariri ujumbe wao wa kampeni kwamba rais huyo wa zamani ni tishio kwa demokrasia.

Kampeni ya Biden ilitumia maoni hayo ya umwagaji damu katika tangazo lililotumwa kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii.

Alimshutumu Trump kwa kuhimiza vurugu za kisiasa.

Kaulimbiu ya kampeni ya Trump, ilisema maoni hayo yalihusu tasnia ya magari na yametolewa kimakusudi nje ya muktadha. **BBC**

# SINGIDA BLACK STAR YATAKA YA SIMBA DAY

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Big Stars imesema lengo lao ni kumaliza tiketi kabla ya kilele cha tamasha lao litakalofanyika Jumamosi, Uwanja wa Liti Singida, kama ilivyofanya Simba ambayo ilimaliza kabla ya siku tatu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Jonathan Kassano, alisema siku hiyo waliyoipachika kwa jina la Singida Big Day', itakuwa ni maalumu kwa ajili ya mashabiki wa soka wa mkoa huo, vitongoji vyake na mikoa ya jirani kukusanyika kwa pamoja kwenye uwanja huo, kupata burudani, na kuwatambua wachezaji wao watakaoichezea timu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano.

"Ni siku kubwa kwa Wanasingida na Watanzania wote, tumejiandaa vizuri sana, tiketi zimeshaanza kuuzwa, hivyo wanataka na kuwakaribisha mashabiki kununua tiketi kwa wingi na sisi tungependa uwanja ujae kabla ya Agosti 10," alisema.

**Jumamosi iliyopita, Simba ilifanya tamasha lao ambalo lilivunja rekodi ya kumaliza tiketi mapema zaidi, siku tatu kabla.**

"Kutakuwa na burudani, mechi ya kirafiki ya kimataifa ambapo tutacheza na timu ya Agle Noir kutoka Burundi, ni timu nzuri imecheza mechi za kimataifa na ni timu kongwe nchini mwao, kabla ya hapo Wanasingida watawatambulisha wachezaji wao wote watakaocheza msimu wa 2024/25, pamoja na 'sapraizi' nyingi tu ambazo tutakuwa nazo, kwa hiyo nawataka mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi ili tusherekee kwa pamoja," alisema.

Timu hiyo ambayo imebadilishwa jina kutoka Ihefu iliyokuwa na maskani yake Mbarali, Mbeya na kuhamia Singida, imesajili wachezaji kadhaa wakiwemo Mohamed Kamara, Edward Manyama, Antony Tra Bi Tra, Ibrahim Imorro, Ayoub Lyanga, Joseph Guede, na wengineo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Afya Kata ya Kwabada wilayani Muheza, Tanga, Andrew Daki (kulia) akiwashukuru wanachama na mashabiki wa klabu ya Yanga kutoka kijiji cha Maduma kwa kufanya usafi katika Zahanati ya Kata ya Kwabada juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# *Dodoma Jiji yatesti mitambo Ligi Kuu*

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Dodoma Jiji, juzi ilijaribu kikosi chake cha msimu wa 2024/25 kwa kucheza dhidi ya Arusha City, ikipata ushindi wa mabao 3-0, mchezo uliopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Katika mechi hiyo, Dodoma Jiji ilichezesha baadhi ya wachezaji iliyowasajili kwa ajili ya msimu ujao akiwemo winga wa zamani wa klabu za Simba, Yanga, Azam FC na Coastal Union, Ibrahim Ajibu.

Mabao ya ushindi yalifungwa na Paul Peter, aliyepachika mawili na Hassan Mwaterema aliyefunga bao moja.

Wachezaji wengine wapya ambao walicheza mechi hiyo kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano ni Waziri Junior, Reliants Lusajo, Ibrahim Ajibu, Heritier Lulihoshi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Daudi Milandu, Dickson Mhilu, Allain Ngeleka, kipa ambaye ni raia wa DR Congo.

Timu hiyo inanolewa na nahodha wa zamani wa timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, na Mtibwa Sugar, Mecky Maxime, ambaye amechukua kikosi kutoka kwa Mkenya, Francis Baraza..

# Aliyepewa 'thank you' arejeshwa Coastal Union

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya kuwa mmoja wa wachezaji wa mwanzo kabisa kuoneshwa mlango wa kutokea na klabu ya Coastal Union, beki wa kati Felly Mulumba amerejeshwa tena kwenye kikosi hicho.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imesema imeamua kumrudisha baada ya kujiridhisha kuwa anaweza kuongeza ubora kwenye kikosi hicho kuelekea kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mulumba, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alikuwa mchezaji kwa kwanza kabisa kupewa 'Thank You', na klabu hiyo, lakini amekuwa mchezaji wa mwisho kusajiliwa msimu huu.

Aliichezea timu hiyo msimu uliopita na kufanya vyema, akiwa pacha na Lameck Lawi, kiasi cha kuiwezesha timu hiyo kukata tiketi ya kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini kuwa moja kati timu zilizokuwa na ukuta imara na kuruhusu mabao machache kwenye Ligi Kuu, ikimaliza nafasi ya nne kwenye msimamo.

Wakati hayo yakiendelea klabu hiyo imetangaza kusajili wachezaji wengine watatu ambao wataisaidia timu hiyo kwenye michuano ya kimataifa.

Wachezaji hao ni straika Banza Kalumba, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo akitokea Tabora United, kiungo mshambuliaji, John Makwata, raia wa Kenya, akitokea klabu ya Zesco ya Zambia na winga Hernest Malonga, raia wa Congo Brazaville, akitokea klabu ya CSMD Diables Noirs ya nchini humo. Ikumbukwe kuwa, Coastal itaanza hatua ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika, dhidi ya Bravos do Maquis ya Angola, Agosti kati ya 16 au 18.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### BERGE AWANIWA MAN U

KLABU ya Manchester United inaweza kujaribu kumsajili kiungo wa kati wa Burnley na Norway, Sander Berge mwenye miaka 26, kwa kumpa mkataba wa kulipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(Sun)***

#### TRIPPIER ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham inavutiwa na beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, huku mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 huko Newcastle United ukiwa bado haujaamuliwa. ***(Telegraph)***

#### OMORODION SAFI CHELSEA

CHELSEA imekubali mkataba wa pauni milioni 35 na Atletico Madrid ili kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Samu Omorodion, na mchezaji huyo mwenye miaka 20 anatazamiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu. ***(Fabrizio Romano)***

#### BROJA KUAMUA HATIMA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Albania, Armando Broja atafanya mazungumzo na kocha, Enzo Maresca kufahamu mustakabali wake. Everton na Wolves ni miongoni mwa wanaomtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

#### CHALOBAH AIVUTIA W'HAM

WEST HAM inavutiwa na mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 26, na beki wa kati wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Borussia Dortmund. ***(Sky Sports)***

#### C. PALACE PIA INAMTAKA

KLABU ya Crystal Palace pia inamtazama mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah, na mlinzi wa Wolfsburg ya Ufaransa, Maxence Lacroix mwenye umri wa miaka 24, kama chaguo la beki wa kati. ***(Telegraph)***

#### CASTLEDINE ATAKIWA

CHELSEA imewasiliana na Rangers kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa akademi yao mwenye umri wa miaka 19, Leo Castledine. Aberdeen pia inavutiwa na mwingereza huyo. ***(FootballScotland)***

#### AVUTIWA ZAIDI DORTMUND

LIVERPOOL bado inavutiwa na mshambuliaji wa Ujerumani na Hoffenheim, Maximilian Beier, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 anataka kujiunga na Borussia Dortmund na yuko kwenye mazungumzo na klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Sky Germany)***

#### BELLA-KOTCHAP AKATALIWA

KLABU ya Southampton imepokea ofa kutoka Hoffenheim kwa mlinzi wa miaka 22, Armel Bella-Kotchap. The Saints hao tayari wamekataa ofa ya pauni milioni 8.6 kutoka Stuttgart. ***(Sky Germany)***

#### DIGNE HAITAKI GALATASARAY

MLINZI wa Aston Villa, Lucas Digne, 31, amekataa pendekezo la kujiunga na Galatasaray. Mfaransa huyo anatarajiwa kubaki na Villa. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL YAJIANDAA KUMBEBA ZUBIMENDI

**LIVERPOOL,** England

### ●●● Imepania kufanya usajili wake wa kwanza chini ya Kocha mpya, Arne Slot, ambaye....

LIVERPOOL inahaha kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi huku wakipania kufanya usajili wao wa kwanza chini ya kocha mpya, Arne Slot.

**Zubimendi alikuwa sehemu ya kikosi cha Hispania kilichoshinda 'Euro 2024' na aliingia katika kipindi cha pili kama mbadala wa Rodri wa Manchester City wakati nchi yake ilipoilaza England 2-1 kwenye fainali.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa Sociedad tangu 2011 na ana kifungu cha kutolewa chenye thamani ya euro milioni 60.

Zubimendi aliisaidia Sociedad kumaliza katika nafasi ya sita kwenye Laliga msimu uliopita, akifunga mara nne katika mechi 31 za ligi.

Klabu hiyo ya Hispania pia ilitinga hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023-24 kabla ya kufungwa na Paris St-Germain.

Zubimendi angekuwa wa kwanza kuwasili chini ya Slot, ambaye alichukua mikoba katika klabu hiyo ya Anfield baada ya kuondoka kwa Jurgen Klopp.

Zubimendi alizungumza hapo awali, mbali na kuvutiwa kwake na mchezaji wa zamani wa Hispania, Xabi Alonso pia anapendelea kucheza nafasi sawa na ya kiungo wa kati aliyokuwa nayo Alonso wakati akicheza.

Alonso pia aliingia katika safu kama mchezaji wa Sociedad kabla ya kujiunga na Liverpool mwama 2004.

Alonso alianza kuiongoza Sociedad B kabla ya kuwa kocha wa klabu ya Bayer Leverkusen ya Ujerumani.



# CHELSEA BADO YAMKOMALIA OSIMHEN

**LONDON,** England

CHELSEA inaamini kuwa kumtaka kwao mshambuliaji wa Atletico Madrid, Samu Omorodion kunaweza kusaidia katika jitihada zao za kumsajili Victor Osimhen wa Napoli, kwa mujibu wa 90min.

The Blues hao wanataka mshambuliaji mpya msimu huu wa majira ya joto na wanakaribia kukamilisha dili la Samu mwenye umri wa miaka 20, baada ya kupata makubaliano na Atletico kufuatia mazungumzo ambayo yatampeleka kiungo Conor Gallagher kutua huko.

Wakati Chelsea inaelekeza nguvu zake katika kuinasa saini ya Samu, vyanzo vimethibitisha kwa jarida la 90min kwamba mazungumzo kuhusu Osimhen bado yanaendelea.

Kuna matumaini ya kumsajili Samu kunaweza kuwasaidia kumpata fowadi huyo wa Napoli.

Samu anaweza kujiunga na kundi ambalo tayari linajumuisha Nicolas Jackson, na kocha Enzo Maresca hivi majuzi alithibitisha kuwa anamwona mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal kama mshambuliaji wa kati bora zaidi.

Napoli wanataka bili ya mishahara ya mshambuliaji wao itolewe kwenye vitabu vyao na Osimhen pia anataka kuondoka, Chelsea inaamini kwamba shinikizo linaweza kuwa kwa upande wa Serie A kukubali ofa yao.

Osimhen na wawakilishi wake wanadaiwa kuchanganyikiwa na mtazamo wa Napoli katika kusajili mshambuliaji mpya kabla ya kumpa ruhusa ya kuondoka na sasa wanashinikiza kuondoka kwa uhamisho wa kudumu.

Chelsea, ingawa nia yao siyo siri, bado haijaonesha dhamira thabiti ya kumsajili Osimhen kwa mkataba wa kudumu.

90min hivi majuzi ili-ripoti kuwa, Napoli iko tayari kupunguza bei hiyo hadi pauni milioni 70 ikiwa dili litajumuisha mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, ambaye analengwa na Napoli kuchukua nafasi ya Osimhen na thamani yake ni pauni milioni 37.

# *Dumfries anaitaka Man United*



**MILAN,** Italia

DENZEL Dumfries anapanga kukataa mazungumzo ya mkataba mpya na Inter Milan hadi baada ya dirisha la usajili la majira ya kiangazi kwani anataka kuhamia Manchester United.

Winga huyo wa pembeni wa Uholanzi yuko katika miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake huko San Siro, ambapo amevutia na kucheza vizuri katika ushindi wa Nerazzurri msimu wa 2023/24 baada ya kujiunga na klabu hiyo kutoka PSV Eindhoven.

Inter inataka kumuongezea muda wa kukaa Milan, lakini Dumfries ameripotiwa kuwa na mawazo mengine.

Kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amepania kutafuta uhamisho msimu huu wa majira ya joto na wazo la kuhamia Old Trafford linamvutia zaidi.

Msitakabali wa Aaron Wan-Bissaka bado unahitaji kupangwa, huku beki huyo wa kulia wa England akitafakari kuhusu uhamisho wa kwenda West Ham United.

Beki huyo wa zamani wa Crystal Palace anavutiwa zaidi na kuhamia Inter, na kuna uwezekano wa kufikia makubaliano ya kubadilishana.

Hapo awali iliripotiwa kuwa Inter inaweza kumnunua Wan-Bissaka, ambaye ana mkataba hadi 2025, ikiwa Dumfries ataondoka.

Kwa bahati mbaya, Dumfries, Mashetani Wekundu wanasemekana kupendelea kumuuza Wan-Bissaka kwa West Ham ili kumsajili Noussair Mazraoui kutoka Bayern Munich.

United wamefungua mazungumzo na wababe hao wa Bundesliga ili kufikia makubaliano ya kumnunua nyota huyo wa kimataifa wa Morocco pamoja na beki wa kati Matthijs de Ligt.

Ombi la pamoja la kuwanunua mabeki hao wawili lilikataliwa wiki iliyopita, huku Mkurugenzi wa Bayern, Max Eberl hivi majuzi akitoa taarifa ya siri kuhusu msitakabali wa De Ligt.

United tayari imemsajili beki Leny Yoro lakini Mfaransa huyo anakabiliwa na takriban miezi mitatu nje ya uwanja baada ya kupata jeraha la mguu katika mchezo wa kujiandaa na msimu uliopita dhidi ya Arsenal. Joshua Zirkzee pia amewasili kutoka Bologna.

# Rodri, Morata wafungiwa UEFA





**PARIS,** Ufaransa

SHIRIKISHO la muungano wa vyama vya soka barani Ulaya, UEFA, limewaadhibu wachezaji wa kimataifa wa Hispania, Alvaro Morata na Rodri, kwa kuwafungiwa mechi moja kwa kuimba kuhusu madai ya kujitawala kwa Gibraltar katika kusherehekea taji la Ubingwa wa Euro 2024.

Shirikisho la soka la Gibraltar limewasilisha malalamiko hayo UEFA mara baada ya Morata, ambaye alikuwa nahodha wa Hispania na kutwaa Ubingwa wa Euro 2024 nchini Ujerumani, na Rodri kuongoza maelfu ya mashabiki kuimba wimbo wa “Gibraltar is Spanish” (Gibraltar ni Hispania) kwenye sherehe, mjini Madrid Julai 14.

Bodi ya nidhamu ya UEFA imewafungia wachezaji hao wawili kwa “kukosa kufuata kanuni za jumla za maadili, kwa kukiuka sheria za msingi za maadili bora, kwa kutumia hafla za michezo kwa udhihirisho wa asili isiyo ya kimichezo na kusababisha mchezo wa mpira wa miguu, na UEFA kudharauliwa.”

Wachezaji wote wawili watakosa mechi ya ufunguzi ya makundi ya Ligi ya Mataifa ya UEFA nchini Serbia Septemba 5.

Gibraltar iko kwenye ncha ya kusini mwa Hispania na imekuwa eneo la Uingereza kwa zaidi ya miaka 300.

## Yanga yaendelea kuinyanyasa Simba

INATOKA UK. 24

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko kadhaa ya wachezaji, lakini hayakuathiri mchezo huo.

Simba ilichezesha wachezaji wake wengi wapya, Joshua Mutale, Debora Fernandes Mavambo, Kelvin Kijili, Augustine Okejepha, Camara, Jean Charles Ahoua, ambao kwa kiasi kikubwa walionyesha utofauti na kikosi cha msimu uliopita.

Kwa upande wa Yanga, iliwachezesha pia nyota wake wapya, Dube, Abuya, na Clatous Chama ambaye anaingia kwenye orodha ya wachezaji waliocheza mechi za dabi wakiwa na timu zote mbili kubwa nchini.

Dakika tano baada ya mapumziko, nusura, Che Malone Fondoh ajifunge mwenyewe, baada ya kupiga kwa kisigino mpira wa krosi ya Pacome, lakini kipa Camara alikaa imara.

Dakika ya 62, Ahoua, alimuacha Yao, na kwenda kupiga krosi iliyounganishwa na Mukwala, lakini kipa Diarra alifanya kazi ya ziada kuupangua na kuwa kona.

Dakika za mwisho Simba walijitahidi kulishambulia lango la Yanga lakini walipoteza nafasi walizozitengeneza ikiwemo ile ya dakika za mwisho.

Kwa matokeo hayo, Yanga inakwenda kucheza fainali dhidi ya Azam FC iliyoifunga Coastal Union mabao 5-2 kwenye mchezo wa mapema jana uwanja wa Amaan Complex Zanzibar. Simba itacheza kusaka mshindi wa tatu dhidi ya Coastal kabla ya fainali hiyo ya Ngao ya jamii siku hiyo hiyo.

## Kanuni 12 mpya zapitishwa

INATOKA UK. 24

Kaizer Chief nchini Afrika Kusini.

Kanuni nyingine iliyopitishwa ni ya ada ya usajili wa wachezaji kutoka nje ya nchi, ambapo sasa klabu zitalazimika kulipa Sh. Milioni Nane, ambapo klabu zenye wachezaji wote 12 wanaoruhiwa kikanuni, zitalazimika kujikamua Sh Milioni 96.

Pia ipo kanuni ya kuwapiga marufuku wachezaji na viongozi kujihusisha na michezo ya kubashiri, yaani 'kubeti', huku ikiwepo kanuni kwamba kila mchezo lazima wawepo wachezaji wawili kutoka timu ya vijana, ambao watakuwa wameorodheshwa kwenye orodha ya wachezaji waliovaa jezi.

Pia ipo kanuni inayowataka makocha wote wakuu wa kigeni nje ya Afrika wawe angalau wana cheti cha ukocha cha 'Pro Diploma', na wasaidizi wa kigeni nje ya Afrika wanatakiwa kuwa na elimu ya 'Diploma A.'

# SIMBU: TUTAPAMBANA KUIPA HESHIMA TANZANIA




**Na Shufaa Lyimo**

MWANARIADHA wa Tanzania, Alphonce Simbu, amesema amejipanga kuhakikisha anaipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye michezo ya Olimpiki inayoendelea katika jiji la Paris, nchini Ufaransa.

Simbu na wanariadha wengine watatu, Gabriel Geay, Jacqline Sakilu na Magdalena Shauri, waliondoka nchini juzi kuelekea kwenye michezo hiyo.

Simbu, ambaye atakimbia kesho pamoja na Geay, alisema kuwa wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri ili kupambania medali.

**"Tunaomba Watanzania waendelee kutuombea, tutajituma na kupambana, binafsi nimejiandaa vizuri ili kuhakikisha ninaitangaza Tanzania katika riadha," alisema Simbu.**

Wakati Simbu na Geay wakitarajiwa kukimbia kesho, wanaridha wa kike, Magdalena na Jacqline wenyewe watakimbia Agosti 11 kwenye kilele cha michezo hiyo.

Wakati huohuo, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Jackson Ndaweka amemuomba Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa, Ali Mwadini kuongoza Watanzania waishio nchini humo kujitokeza kwa wingi kuwashangilia wanariadha hao.

Ndaweka, alitoa ombi hilo juzi asubuhi wakati alipomtembelea na kupeleka taarifa ya ushiriki wa nchi ya Tanzania katika mashindano hayo kupitia mchezo wa riadha.



Wachezaji wa mpira wa Kikapu wa timu ya Vijana ya Dar es Salaam, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mdogo wa Msuva aibukia KenGold FC*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KenGold imemsajili winga wa KMC, James Msuva, kwa ajili ya kuichezea timu hiyo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imesema Msuva ni mmoja wa wachezaji watakaoichezea timu hiyo, itakayocheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kupanda msimu huu.

Msuva, ambaye ni mdogo wa winga wa timu ya taifa ya Tanzania, Simon Msuva. Mbali na kuichezea klabu ya KMC, amewahi pia kuichezea klabu ya Mbao FC.

"Nina furaha kuwa sehemu ya familia ya KenGold, kila timu inayoingia kwenye Ligi Kuu inakuwa na malengo yake, na sisi pia tunayo ya kwetu, lakini makubwa ni ya klabu kuona inafanya vyema na inabaki kwenye ligi ikiwa kwenye nafasi nzuri, naamini kwa kikosi kilichopo na mazoezi tunayofanya tutafanya kitu ambacho wengi hawawezi kutarajia kwa sababu ni timu iliyosheheni vijana wengi wenye ari na vipaji," alisema Msuva.

Mbali na hilo, klabu hiyo pia imefanikiwa kumsajili mshambuliaji wa wa TMA Stars, Ramadhan Chobwedo, ambaye alikuwa mmoja wa waliofunga mabao mengi kwenye Ligi ya 'Championship' msimu uliomalizika.

KenGold imeshinda vita ya kumuwania mshambuliaji huyo aliyekuwa akitakiwa kwa udi na uvumba na Prisons.

"Nimefurahi sana kwa kusajiliwa na KenGold. Nipo hapa kuitetea nembo ya klabu hii, na ninawaahidi mashabiki wa timu kuwa tutapambana sana, japo ni wageni kwenye ligi lakini lengo letu ikiwezekana ni kuchukua moja kati ya nafasi nne za juu, na ikishindikana kabisa basi tubaki kwenye ligi tukiwa kwenye nafasi nzuri," alisema mshambuliaji huyo.

# Michezo

Ijumaa Agosti 9, 2024

Nipashe




Liver yajiandaa kumbeba Zubimendi UKURASA 21



Mshambuliaji wa Simba, Edwin Balua (kulia) akiwatoka wachezaji wa Yanga, Clement Mzize (aliyeshika chini) na Shedrack Boka, katika mchezo wa nusu fainali Ngao ya Jamii kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **NA MPIGA PICHA WETU**

# YANGA YAENDELEA KUINYANYASA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Yaibuka na ushindi na kutinga fainali Ngao ya Jamii, uso kwa uso na Azam...

BAO lililolofungwa na kiungo mshambuliaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Maxi Nzengeli liliwapeleka Yanga fainali ya Ngao ya Jamii kwa kuifunga Simba bao 1-0 katika mchezo mkali na wa kusisimua uliochezwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga imelipa kisasi cha kufungwa kwa mikwaju ya penalti 3-1 katika mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii msimu uliopita kwenye uwanja wa Mkwakwani Tanga, baada ya kutoka suluhu dakika 90 za mchezo, lakini pia imeendelea kuinyanyasa Simba katika mechi nne walizokutana ndani ya misimu miwili, Yanga wamepata ushindi kwenye michezo mitatu , miwili ya Ligi Kuu msimu uliopita na wa jana wa Ngao ya Jamii huku Simba ikipata ushindi kwenye mchezo kama wa jana, msimu uliopita.

Mechi ya jana ilianza kwa kasi na dakika ya kwanza tu, Simba ilifika langoni mwa Yanga, Shomari Kapombe akiambaa kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi iliyokuwa ikielekezwa kwa Steven Mukwala, lakini iliishia mikononi mwa mwa kipa Djigui Diarra.

**Yanga ilikosa bao la wazi dakika moja baadaye pale Prince Dube alipobaki na kipa Moussa Camara, akampeleka upande wa kulia, lakini mpira uligonga nguzo na kurejea uwanjani kabla ya kuokolewa na mabeki wa Simba.**

Dube aliathiriwa zaidi na kipa Camara baada ya kutoka hatua kadhaa na kulibana lango, lakini angeweza kufunga kama angeufutilia mpira uliogonga mwamba na kurejea kama asingekuwa na haraka ya kutaka kukimbilia kwenye kibendera cha kona kushangilia.

Kasi ya mechi hiyo iliendelea dakika za mwanzo, kwani dakika ya tano ya mchezo, Mukwala alimpokonya mpira Yao Kouassi pembeni karibu na lango la Yanga, lakini badala ya kutoa 'krosi pasi' kwa wenzake, akataka kufunga kwenye upande mgumu na mpira ukatoka nje.

Baada ya hapo mechi ilitulia na timu zikawa zinashambuliana kwa zamu, ilikuwa dakika ya 26 ambapo Nzengeli aliachia shuti la mbali lililopaa juu ya lango. Mohamed Hussein 'Tshabalala', alilazimika kuutoa mpira nje kuwa kona baada ya krosi ya Shadrack Boka kuleta kizaazaa langoni.

Nzengeli alirejea tena langoni mwa Simba dakika mbili kabla ya mapumziko, akiwa hatua chache tu kutoka langoni alipenyezewa pasi kutoka kwa Dube, lakini shuti lake lilitoka pembeni ya lango.

Hatimaye alisawazisha makosa yake dakika mmoja baadaye, ikiwa ni dakika moja kabla ya kwenda mapumziko, alipoukwamisha mpira wavuni kutokana na uzembe wa mabeki wa Simba kumuacha akiwa huru karibu kabisa la lango.

Wachezaji wa Yanga walipigiana pasi nyingi karibu na lango la Simba, kabla ya mpira kupelekwa kwa Nzengeli ambaye aligeuka na kutazamana ana kwa ana na kipa Camara, kabla ya kuachia shuti kali la mguu wa kushoto lililotinga nyavuni.

INAENDELEA UKURASA 23

# Kanuni 12 mpya zapitishwa, viashiria ushirikina faini mil. 20

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imepitisha kanuni 12 mpya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya msimu wa 2024/25 unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Taarifa iliyotolewa na TFF imesema kuwa, kamati hiyo ilipitisha kanuni hizo, Agosti Mosi, baada ya kujadili na kufanyia kazi maoni ya wadau mbalimbali wa soka kwa ajili ya kanuni mpya za ligi.

Taarifa imesema kuwa kanuni zilizofanyiwa maboresho na kupitishwa katika kikao hicho ni pamoja na kanuni ya saba ya 'firts league' kuhusu nane bora, kanuni ya tisa ya ligi kuhusu uwanja, kanuni ya 17 kuhusu taratibu za mchezo, kanuni ya 31 kuhusu timu kutofika uwanjani, kanuni ya 47 kuhusu udhibiti wa klabu, kanuni ya 62 kuhusu wachezaji wa kigeni, kanuni ya 77 kuhusu makocha na kanuni ya 79 kuhusu maamuzi yasiyokatiwa rufaa.

Baadhi ya kanuni mpya ni ya viashiria vya kishirikina uwanjani, ambapo badala ya fainli ya Sh. 500,000, mpaka Sh. Milioni Moja, sasa timu zitakazobainika kufanya vitendo vinavyoashiria ushirikina, zitatozwa faini ya kati ya Sh. Milioni Tano hadi Milioni10, lakini kama hali hiyo ikionekana inajirudia, klabu itapigwa faini ya Sh. Milioni 20.

Ikumbukwe, Mei mwaka 2022, klabu ya Simba ilitozwa faini ya dola za marekani 10,000 (zaidi ya Shilingi milioni 23) kwa kuonyesha viashiria vya vitendo hivyo vya kishirikina kwenye mchezo wao wa robo fainali kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >